# Nchi Yetu

Toleo na. 865

## Jarida Maalum *la Miaka 60 ya Muungano*



MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

1964-2024



**Bodi ya Wahariri:**

**Mwenyekiti**
Mobhare Matinyi
Mkurugenzi wa Idara ya Habari
(Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali.

**Wajumbe**
Rodney Thadeus
Jonas Kamaleki
Lilian Lundo
Ahmed Sagaff

**Msanifu**
Kelvin Nicomedius Kanje



***Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,***
Idara ya Habari (Maelezo)
Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole,
S.L.P. 677; Dodoma, Tanzania
Simu: +255 22 292192,
Barua pepe: maelezo@mawasiliano.go.tz
Tovuti: www.maelezo.go.tz



*Tufuatilie katika kurasa zetu kwenye mitandao ya jamii*
/ Msemaji Mkuu wa Serikali
/Maelezo News


# Neno la Utangulizi

## *Miaka 60 ya kujivunia utaifa wetu*


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi ya kipekee barani Afrika na ulimwenguni kote, sasa imetimiza miaka 60 tangu ilipoasisiwa mnamo tarehe 26 Aprili, 1964.
Waasisi wa Tanzania tunayoijua hivi leo walikuwa viongozi wetu wawili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika, na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani mashujaa wetu hawa.
Leo tunapotimiza miongo sita tuna mengi ya kukumbuka, kujifunza, kujipongeza na kujivunia kama taifa huku tukitambua kwamba fahari ya kuwa taifa moja inatutaka tuulinde muungano huu, tuutunze, tuutetee na tuupiganie kwa nguvu na akili zetu zote.
Kwa hakika kufikisha muda huu tukiwa bado ni taifa moja ni hadithi ya mafanikio; hivyo basi, hatuna budi kupima ni wapi tumefanya vizuri na ni wapi panahitaji juhudi zetu zaidi na maarifa.
Jarida hili la NCHI YETU linapitia baadhi tu ya mafanikio yetu ili tuone tumefikaje hapa tulipo; na tunakwendaje huko mbele huku tukizingatia nguzo kuu nne zilizomo katika falsafa ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nguzo hizo nne ni maridhiano, upatanishi, mabadiliko na kujenga upya taifa letu, zikimaanisha sisi Watanzania tufanya mabadiliko ili tulijenge upya taifa letu linalo-heshimu upatanishi ili siku zote sisi wote tuishi kwa amani.

*Mungu ibariki Tanzania;*
*Mungu ibariki Afrika.*



Bw. Mobhare Matinyi
Mkurugenzi wa Idara ya Habari MAELEZO
na Msemaji Mkuu wa Serikali

# NDANI *ya* JARIDA





Yaliyomo

003 **Miaka 60 ya Muungano:** *Hotuba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Kuadhimisha Miaka 60 ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 25 Aprili, 2024, Dodoma*

006 **Miaka 60 ya Muungano:** *Tanzania Yanufaika Sekta ya Biashara na Uwekezaji Kimataifa*

010 **Sekta ya Elimu Yawa Kiungo Muhimu** *katika Muungano*

NDANI YA MIAKA 60...

012 **Jaji Warioba Ataja** *Siri ya Muungano Kudumu*

013 **Miaka 60 ya Muungano:** *TRA Ilivyoboresha Ukusanyaji wa Mapato*

017 *Mafanikio Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika* **Miaka 60 ya Muungano**

019 **Miaka 60 ya Muungano** *na Ongezeko la Majaji Mahakama ya Rufani Tanzania*

021 *Mafanikio ya Bunge la Tanzania katika* **Miaka 60 ya Muungano**

NDANI YA MIAKA 60...

028 *NIDA Yafungua Ofisi 153* **Tanzania Bara, Zanzibar**

030 **TANESCO, ZECO** *Kuongeza Wigo wa Ushirikiano*

032 *Usahihi wa Utabiri Hali ya Hewa Nchini* **Wafikia Asilimia 98**


036 *Mafanikio ya Tasnia ya Takwimu katika* **Miaka 60 ya Muungano**

041 *Msuya, Malecela na Mongella Watoa Neno Muungano* **Kutimiza Miaka 60**










**NCHI YETU**

Toleo Maalum la Jarida la Nchi Yetu tukiwa tunatimiza Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*Picha na Idaya ya Habari -MAELEZO*


046 **Uchumi wa Jeshi,** *Maslahi ya Wanajeshi Yaboreshwa*

048 *Kamati ya Pamoja SMT, SMZ Nguzo Muhimu kwa* **Uhai wa Muungano**

050 *Ijue* **Misingi ya Muungano** *wa Tanganyika na Zanzibar*


**NDANI YA MIAKA 60...**


054 **Miaka 60 ya Muungano** *Yazipa Nguvu Sekta za Viwanda na Biashara*

058 **Miaka 60 ya Muungano** *Imewanufaisha Watanzania Kijamii, Kimazingira, Kisiasa na Kiuchumi*

064 **Tuna Kila Sababu ya Kujivunia Muungano** *- Rais Samia*





Tembelea tovuti yetu, www.maelezo.go.tz

# *Kutoka kwa Rais,* Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

Na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hsaan

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa tarehe 26 mwezi wa nne mwaka 1964 ikiwa ni Muungano wa hiari wa nchi mbili huru: Jamhuri ya Tanganyika chini ya uongozi wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ikiongozwa na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.

Kila ninapopata fursa ya kuzungumzia Muungano wetu, fikra zangu hutawaliwa na picha ya vijana wanne kutoka pande zote mbili za Muungano. Vijana hao, wawili wa kiume na wawili wa kike, waliomsaidia Mwalimu Julius Nyerere kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar kutoka kwenye vibuyu viwili tofauti, kwa kuumimina kwenye chungu kimoja, kitendo kilichoashiria kuundwa kwa Taifa jipya, yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jinsi udongo ulivyo, ni vigumu sana kuuchambua na kuweza kuutenganisha uliotoka Zanzibar na ule uliochotwa Tanzania Bara. Baada ya kuuchanganya, hakuna teknolojia inayoweza kuurudisha udongo ule kwenye hali yake ya awali katika vibuyu viwili tofauti. Kwa maana nyingine, kitendo cha kuchanganywa kwa udongo kiliashiria dhamira ya kujenga muungano wa kudumu.

Muungano wetu ni maalumu na wa kipekee, uliojengwa katika misingi ya utu, udugu, na umajumui wa Afrika (Pan-Africanism), umeweza kushinda majaribu mengi ya kuuvunja, na vilvile umefanikiwa kudumu hadi sasa. Nchi nyingi ziliwahi kufanya majaribio ya kuungana, bila ya mafanikio. Katika kuelezea upekee wa Muungano huu, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema maneno yafuatayo, naomba kunukuu: ***"Tanzania ni lulu ya pekee kabisa katika historia ya Afrika huru. Nchi nyingine zote ni za kurithi kutoka katika Ukoloni. (Lakini) Tanzania ni ya kuundwa na sisi wenyewe, kwa hiari yetu wenyewe, baada ya kukomboa sehemu (zote mbili za Muungano) kutoka katika Ukoloni."*** Kwa upande wake, Sheikh Abeid Amani Karume akiuzungumzia Muungano huu, aliwahi kusema, nanukuu *"Muungano wa Tanganyika na Zanzibar una thamani kubwa kwetu sisi Waafrika".*

Inawezekana baadhi ya Watanzania wakajiuliza, iliwezekanaje Muungano huu ukawepo, na umewezaje kudumu miaka yote hii? Majibu ya maswali hayo ni muhimu kwa kutambua kwamba zaidi ya robo tatu ya Watanzania wa leo, wamezaliwa baada ya Muungano. Maelezo kuhusu maswali hayo yapo mengi, lakini kwa muktadha wa leo nitazungumzia mambo makubwa matatu yaliyoufanya Muungano wetu udumu na kuimarika.



Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akishiriki Sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2024 katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam.

Katika kipindi cha uhai wa Muungano, wananchi wamehama au kuhamia kutoka upande mmoja wa Muungano kwenda upande mwingine. Wamejenga, wameoa na kuolewa na kuleta kizazi cha watanzania, wanaendesha shughuli zao za maisha bila ya kubughudhiwa.

Muingiliano wa shughuli za kijami na kiuchumi umeongeza kasi kwa wananchi kutembeleana kwa wingi. Kuna wanaosafiri kwa majahazi kutoka Unguja na Pemba kwenda Pangani, Mkwaja, Saadani, Bagamoyo, Mafia, Kilwa na kadhalika; na wapo wanaotoka Pwani ya Bara na kuingia Zanzibar kupitia bandari za Fuoni, Kizimkazi, Fumba, na Mkokotoni. Vilevile, kuna wanaotumia boti za kisasa au ndege pia. Wote hao, bila Muungano, wangelazimika kusafiri kwa utaratibu mgumu zaidi ambao huenda ungehusisha kutafuta visa, kutumia hati za kusafiria na hata kupata vibali vya ajira upande wowote ule wa Muungano.

Sababu nyingine ya Muungano wetu kudumu ni uwepo wa Tume ya Pamoja chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, inayosikiliza na kutatua changamoto za Muungano kila zinapojitokeza. Katika ya mwaka 2021 hadi sasa, hoja 15 kati ya 18 zimeshapatiwa ufumbuzi. Tume hiyo inafanya kazi kubwa ya kulinda dhamira ya dhati ya kuudumisha Muungano wetu.

Ni wajibu wetu kuendelea kuweka mazingira mazuri zaidi ya watu kushirikiana, kujenga umoja na mshikamano wa Kitaifa, ili Muungano wetu udumu vizazi hadi vizazi na kuleta manufaa zaidi kwa watu wetu.



Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akishiriki Sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 2024 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Pamoja na kuwaunganisha wananchi na kuimarisha mahusiano mazuri, Muungano umetuwezesha kulinda Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, lakini pia kwa umoja wetu, na kupitia jeshi letu, tumeweza kulinda mipaka ya taifa letu. Ninafuraha leo kuwahakikishia kwamba, mipaka yetu, uhuru wetu, na mapinduzi yetu, vyote viko salama ndani ya Muungano wetu.

***Ili tuweze kujenga Muungano ulio imara zaidi, Serikali immekuja na falsafa ya maridhiano, kustahimiliana, tuweze kubadilika, na kwa pamoja tujenge upya Taifa letu (maarufu kama R4).*** Kupitia falsafa hio, tumefanya mapitio ya mfumo wa haki jinai; kuhakikisha uhuru wa kujieleza,na vyama vya siasa kufanya shughuli zao kwa uhuru. Aidha, kupitia mazungumzo na ushirikishwaji, tumefanya mabadiliko kwenye sheria zetu za uchaguzi, sheria ya vyama vya siasa na sheria ya Tume ya Uchaguzi.

***Katika diplomasia,*** Muungano umeiwezesha Tanzania kuwa na ushawishi mkubwa zaidi kikanda na kimataifa. Tumeweza kunufaika na kukuza uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine, na Nchi yetu na Taasisi za Kimataifa kwa manufaa ya pande zote za Muungano.

***Sensa ni moja kati ya mambo ya Muungano.*** Hadi sasa, zimefanyika sensa za watu na makazi mara 6, Sensa ya kwanza ilionesha Tanzania kuwa na watu Milioni 9.6 na ile ya mwisho ya 2022 imetuonesha idadi ya Watanzania kuwa milioni 61.741. Taarifa hizi za Sensa zina msaada mkubwa kwa mipango ya kiserikali., na kutuongoza katika matumizi ya rasilimali, na kuimarisha uwakilishi wa wananchi.

***Katika Elimu,*** mazingira mazuri yaliyojengwa na Muungano wetu yamewezesha wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu kupata elimu bila ubaguzi. Itakumbukwa kuwa baada ya uhuru, chuo kikuu pekee kilikuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Zanzibar haikuwa na Chuo Kikuu. Kupitia Muungano, vijana wa Kizanzibari walipata fursa ya elimu ya juu katika Chuo hicho na vyuo vingine Tanzania Bara.

Ninafarijika kwamba, miaka 60 baada ya Muungano tunavyo vyuo vikuu 49 vikiwemo 19 vya umma na 30 vya binafsi. Kati ya vyuo hivyo, 46 viko Tanzania Bara na 3 viko Tanzania Zanzibar. Vyuo hivi vinatoa fursa za masomo kwa wanafunzi kutoka pande zote za Muungano, ambapo kwa Mwaka 2023/24, kulikuwa na jumla ya wanafunzi wa elimu ya juu 240,523, ikilinganishwa na wanafunzi 14 tu waliokuwepo wakati nchi zetu zinaungana.

** Wajibu wetu ni kuendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili viendelee kutimiza jukumu la kulinda mipaka na usalama wa raia na mali zao kwa ufanisi mkubwa.*

***Suala la usawa wa kijinsia*** limepewa umuhimu katika Muungano tangu siku ya kwanza ya Muungano wenyewe. Kama nilivyoeleza hapo awali kuhusu vijana wa kike na wa kiume walioshiriki kwenye kuchanganya udongo.

Hii ilikuwa ni ishara kwamba, Muungano wetu ulidhamiria kujenga Taifa lenye usawa. Suala la usawa wa kijinsia zote liliingizwa kwenye Katiba, hatua iliyowezesha uwakilishi wa wanawake Bungeni kuongezeka kutoka watatu tu mwaka 1964 wakati wa Bunge la kwanza la Muungano, hadi sasa kufikia wabunge wanawake 148 sawa na 37.75% ya wabunge wote 392 tulionao sasa. Aidha, wakati huo, hapakuwa na mwanamke yeyote kwenye uongozi wa mihimili ya dola, yaani Serikali, Bunge na Mahakama. Leo hii, kati ya mihimili mitatu ya dola, wanawake wanaongoza mihimili miwili, Serikali na Bunge, jambo linalothibitisha kuendelea kuimarika kwa usawa wa kijinsia.

***Katika kipindi cha miaka 60, nchi yetu imeendelea kuimarisha Mawasiliano kupitia vyombo vya habari, simu za mkononi na mitandao ya kijamii.*** Wakati tunaungana njia kuu za Mawasiliano za haraka tulizokuwa tukitegemea ni simu za mezani na zilikuwa katika familia chache sana. Leo hii kupitia Muungano wetu tumeweza kuimarisha mawasiliano, na hadi sasa takriban kila familia ina mtu mwenye simu ya mkononi na watoa huduma za simu wameongezeka.

Kwa wananchi wenzangu, kama nilivyosema mara kadhaa, ninarudia kusema kwamba, ***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja tu ulimwenguni, na ndio inayozaa Watanzania. Jamhuri hiyo ni yetu na Tanzania ndio kwetu hatuna kwengine katu, abadan. Ninawasihi kudumisha uzalendo kwa kuzidisha umoja na mshikamano wa Kitaifa.*** Tukifanya hivyo, tutaweza kuurithisha Muungano huu kwa vizazi vyetu, ukiwa imara zaidi.






Maonesho ya kwata ya kikundi cha Askari wa Jeshi la Polisi Tanzania, kutoka Zanzibar, maarufu kama Askari wa Tarabushi, wakionesha maonesho mbalimbali ya aina ya kwata tangu kipindi cha utawala wa Sultan na kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Askari hao walijipatia umaarufu mkubwa kutokana na uvaaji wa kofia za Tarabushi. Onesho hilo lilifanyika katika kilele cha Sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 2024.



# Miaka 60 ya Muungano: *Tanzania Yanufaika Sekta ya Biashara na Uwekezaji Kimataifa*



**45**
**Jumla ya Balozi na Ofisi za Uwakilishi**

**05**
**Jumla ya Konseli Kuu**

Na Jonas Kamaleki, Maelezo

Katika miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sekta za biashara na uwezekaji zimefaidika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa shughuli zake pamoja na kusainiwa kwa mikataba ya miradi mbalimbali ya pamoja baina ya Tanzania na nchi zingine duniani.

Ushirikiano wa uwili kipitia mikataba ya pande mbili umewezesha utekelezaji wa miradi ya barabara, maji, reli, bandari na viwanja vya ndege nchini. Mathalani, Zanzibar imenufaika na miradi ya ukarabati wa miundombinu ya maji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 92.18 kutoka India.

Zaidi ya hapo, India imetoa mikopo mingine ya masharti nafuu ya jumla ya dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza maji katika miji 24 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Aidha, serikali imeendelea kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya miundombinu ya uchukuzi, maji na nishati kutoka serikali ya Japan inayotokelezwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japan (JICA) nchini Tanzania ikiwemo mradi wa Maendeleo ya Soko la Samaki Malindi huko Zanzibar wenye thamani ya takribani shilingi bilioni 19.610 uliokamilika mwaka 2023.

Mradi mwingine ni ule wa Uboreshaji Uwezo wa Usafirishaji jijini Dar es Salaam uliogharimu takribani shilingi bilioni 22.482 na kukamilika mwaka 2023 pia.
Haya yote yalibainishwa hivi karibuni na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Balozi Mbarouk Nassoro Mbarouk, wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yake katika miaka 60 ya muungano.

Aliongeza kwa kutaja mradi wa upanuzi wa barabara mpya ya Bagamoyo awamu ya pili ya kipande cha Morocco hadi Mwenge chenye urefu wa kilomita 4.3 uliogharimu takribani shilingi bilioni 81.350 na mradi wa usambazaji maji mjini Zanzibar uliogharimu takribani shilingi bilioni 217.3 ulioanza mwaka 2022 ukitarajiwa kukamilika mwaka 2027.



*TZS Bilioni*

**19.610**

Gharama za mradi wa 'Maendeleo ya Soko la Samaki Malindi, Zanzibar uliokamilika mwaka 2023

*TZS Bilioni*

**81.350**

Gharama za mradi wa upanuzi wa barabara mpya ya Bagamoyo awamu ya pili (kipande cha Morocco-Mwenge) chenye urefu wa kilomita 4.3

*TZS Bilioni*

**22.482**

Gharama za mradi Uboreshaji Uwezo wa Usafirishaji jijini Dar es Salaam uliokamilika mwaka 2023

*TZS Bilioni*

**217.3**

Gharama za mradi wa usambazaji maji mjini Zanzibar

Aidha, katika kuimarisha ushirikiano wa uwili, Tanzania na nchi marafiki zimekuwa zikitafuta ufumbuzi wa vikwazo visivyo vya forodha (NTBs) kwa lengo la kuimarisha biashara. Mathalani, kuanzia mwaka 2007 mpaka 2023 Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zimefanikiwa kuondoa zaidi ya vikwazo 309 vinavyoathiri biashara katika nchi zao.

Tanzania imesaini makubaliano mbalimbali pamoja na kutatua vikwazo visivyo vya kibiashara vinavyokwamisha ufanyaji wa biashara na usafirishaji wa mizigo na abiria baina ya Tanzania na nchi hizo. Katika kipindi hiki, Tanzania imefanikiwa kuwa sehemu ya kuanzishwa kwa jumuiya za kikanda ambapo ilishiriki kuanzisha Umoja wa Afrika AU); Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Kimataifa ya Kanda ya Maziwa Makuu (ICGLR).

Balozi Mbarouk alibainisha zaidi kuwa Tanzania imefanikiwa kuwa sehemu ya utekelezaji wa dhana ya kutatua changamoto za kidunia kwa pamoja, yaani 'multilateralism', imefanikiwa kuwa mbia anayeaminika na kukubalika katika maamuzi mbalimbali duniani hasa katika mashirika ya kimataifa hususan Umoja wa Mataifa.

Tanzania imekuwa ni mbia katika maamuzi kwenye vyombo mbalimbali ikiwemo Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA); Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC); Shirika la Biashara la Dunia (WTO) na Benki ya Dunia.

Tanzania imekuwa sehemu ya maamuzi katika maeneo ya mazingira na mabadiliko ya tabia nchi; ulinzi na usalama; utatuzi wa migogoro; maendeleo endelevu na utafutaji rasilimali kwa ajili ya maendeleo. Tanzania imepata fursa ya kutoa msimamo wake kwa masuala muhimu ikiwemo misimamo kuhusu mgogoro wa Israel na Palestina; suala la Sahara Magharibi na Jamhuri ya China kurejeshewa uanachama wake Umoja wa Mataifa.

> “Katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, Zanzibar imenufaika na miradi ya ukarabati wa miundombinu ya maji yenye thamani ya dola za Marekani milioni 92.18 kutoka India.

Nchi hii imekuwa sehemu ya kuunga mkono Sera ya kutofungamana na Upande wowote (NAM) na kuunga mkono ajenda ya msimamo wa Kundi la 77 na China katika majukwaa ya Kimataifa kwa maslahi mapana ya Taifa.

Tanzania imekuwa ikishiriki katika kulinda amani kupitia misheni za kikanda ikiwemo EAC, SADC, AU na UN.

Baadhi ya maeneo ambayo Tanzania imechangia walinda amani ni pamoja na nchi za Lebanon, Sudan Kusini, Sudan, Liberia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Msumbiji na Afrika ya Kati. Aidha, kwa upande mwingine, Tanzania imeshiriki kikamilifu katika utatuzi wa migogoro kwa njia ya mazungumzo na diplomasia kwenye nchi na maeneo mbalimbali.

Muungano umeiwezesha Tanzania kuwa sehemu salama ya kutatua changamoto ya wakimbizi ambapo serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuunga mkono juhudi za UN za kutafuta suluhisho la kudumu kwa wakimbizi.

Kupitia miaka 60 ya muungano, Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa taasisi za kimataifa kama ishara mojawapo ya kuaminika na kukubalika na nchi zingine. Miongoni mwa taasisi na mashirika ya kimataifa yenye makao makuu hapa nchini ni pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki; Mahakama ya Afrika Mashariki; na Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Taasisi zingine ni Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika; Taasisi za Umoja wa Mataifa; Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa; Chuo cha Upasuaji cha Afrika Mashariki, Kati na Kusini; Umoja wa Posta Afrika; Mahakama ya Kimataifa ya Masalia ya Kesi za Mauaji ya Kimbari ya Rwanda; na Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha SADC.

Uhusiano kati ya Tanzania na nchi mbalimbali umeendelea kuimarika. Tanzania imeendelea kufungua balozi na ofisi za uwakilishi katika nchi mbalimbali za kimkakati ikiwa ni sehemu ya kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje kwa ujumla inayosisitiza kuhusu Sera ya Diplomasia ya Uchumi.

Serikali ya Awamu ya Sita imefungua balozi mpya mbili nchini Austria na Indonesia na konseli kuu mbili za Lubumbashi nchini DRC na Guangzhou nchini China. Ufunguzi wa balozi hizo umeifanya Tanzania kufikisha jumla ya balozi na ofisi za uwakilishi zipatazo 45 na konseli kuu tano.

Tanzania ni mwenyeji wa nchi na mashirika ya kimataifa zaidi ya 90 ikiwemo konseli kuu ambazo baadhi yake zina ofisi ndogo Zanzibar kama vile China, Oman, India na Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE). Uwepo wa konseli kuu umechangia kuimarika kwa ushirikiano wa uwili, ujirani mwema na kuongezeka kwa manufaa katika sekta za ushirikiano ikiwemo biashara, utalii, uwekezaji, uchumi wa buluu na kuieneza lugha ya Kiswahili kama bidhaa.

Tanzania imefanikiwa kutoa viongozi mahiri kuongoza taasisi za kikanda na kimataifa ikiwa ni ishara ya kuaminiwa na mataifa mengine ikiwemo uteuzi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Mwenyekiti Mwenza wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Afrika utakaofanyika Paris, Ufaransa, mwezi Mei 2024.

Aidha, Tanzania pia ilitoa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo Dkt. Salim Ahmed Salim aliongoza vikao vinne vya Baraza hilo mwaka 1979 na 1980. Vilevile, Dkt. Salim alihudumu kama Katibu Mkuu wa Umoja wa Afrika (AU) ambapo wakati huo ulikuwa Umoja wa nchi Huru za Afrika (OAU); Dkt. Asha-Rose Migiro kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa kwanza kutoka Afrika; Balozi Getrude Mongela kuwa Rais wa Bunge la Afrika; Dkt. Stergomena Tax kuwa Katibu Mtendaji wa SADC; Balozi Liberata Mulamula kuwa Katibu Mtendaji wa kwanza wa ICGLR; na Balozi Juma Mwapachu kushika wadhifa wa Katibu Mkuu wa EAC.

Watanzania wengine ni Profesa Anna Tibaijuka kuwa Naibu Katibu Mkuu na Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-HABITAT) na pia Mkuu wa Ofisi za Umoja wa Mataifa Nairobi (UNON); na kadhalika Joyce Msuya kuwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa muda wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) na hivi sasa Katibu Mkuu Msaidizi wa Masuala ya Kibinadamu na Naibu Mratibu wa Huduma za Dharura.

Wengine ni Elizabeth Mrema kushika hivi sasa wadhifa wa Katibu Mkuu Msaidizi wa UN na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); na hivi karibuni Spika wa Bunge la Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb.) kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge ya Dunia (IPU) akiwa mwanamke wa kwanza kutoka barani Afrika kushika wadhifa huo.

Tanzania imechangia katika juhudi za kubidhaisha lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi ikiwemo kutoa ushawishi wa matumizi ya lugha hii kama nyenzo ya diplomasia, usuluhishi wa migogoro; ukombozi na uhuru katika nchi za bara la Afrika.

Aidha, Kiswahili kuwa lugha rasmi AU, EAC na SADC kufanikiwa kuishawishi dunia kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambapo imeitambua tarehe 7 Julai ya kila mwaka kama siku ya lugha ya Kiswahili kimataifa. Tanzania kupitia balozi zake imewezesha kuanzisha madarasa na vituo vya lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali ikiwemo Uholanzi, Ethiopia na Korea Kusini.

Serikali imefanikiwa kuimarisha ushiriki wa Watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) na raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania katika maendeleo ya taifa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni serikali kuchukua hatua za kisera kwa kujumuisha masuala ya diaspora katika mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001.

Serikali iko katika hatua za kukamilisha kutoa hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania ili kuwawezesha kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya taifa. Mchakato huo unatarajiwa kukamilika baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kufanya marekebisho ya sheria za ardhi na uhamiaji.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa mwanadiplomasia namba moja, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itaendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano huo sambamba na kuendelea kutetea, kulinda na kudumisha usalama na amani duniani kwa kushirikiana na jumuiya ya kimataifa.

# Sekta ya Elimu *Yawa Kiungo Muhimu katika Muungano*

Na WyEST

Wakati Tanzania inatimiza miaka 60 ya muungano, sekta ya elimu inajivunia mafanikio makubwa katika ngazi zote za elimu, hususani katika kuleta mageuzi makubwa ya kisera Tanzania Bara na Zanzibar.

Pamoja na kuwa elimu ya juu pekee ndiyo ipo chini ya muktadha wa muungano, lakini kumekuwa na ushirikiano mkubwa kiutekelezaji katika ngazi zote za elimu.

Dunia nzima hivi sasa iko katika harakati za kuleta mabadiliko katika mifumo ya utoaji elimu kupitia mabadiliko ya sera na mitaala kwa lengo la kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi, ambayo ndiyo msingi mkuu wa kuleta mabadiliko katika taifa.

Tanzania katika sura ya muungano imefanya maandalizi ya pamoja na sasa Tanzania ina sera na mitaala ya elimu imara kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa upande wa Tanzania Bara na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa upande wa Zanzibar.

Pamoja na kuimarisha sera, miundombinu ya elimu haikuachwa nyuma ambapo Tanzania inajivunia ujenzi wa kampasi kubwa ya kisasa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) na Taasisi ya Sayansi za Bahari, Zanzibar.

Kampasi hii ya Zanzibar inalenga kuendelea kutoa mafunzo, utafiti na ushauri katika eneo la sayansi za bahari ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa uchumi wa buluu ambao ni mwelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika juhudi za kuinua uchumi wa Tanzania.

Kampasi hiyo ya Zanzibar itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 wa shahada za awali na 50 wa shahada za uzamili.

Katika muktadha huo huo wa kimuungano, leo tunashuhudia wanafunzi wa elimu ya juu wakiwa na nafasi na kuchaguliwa katika vyuo vikuu vya bara na Zanzibar bila kujali anatoka upande upi wa muungano.

### *Miradi kupitia Mfuko wa Elimu (TEA)*

Kazi hii ya uimarishaji elimu katika pande zote imeendelea kufanyika katika muktadha wa muungano ili Watanzania wote wapate fursa mbalimbali za elimu na mafunzo ikiwemo mafunzo ya amali.

**49,063**


**Jumla ya vijana walionufaika na Programu ya ESPJ chini ya Benki ya Dunia na SJMT**

**46%**

**Wanawake 22,413 walionufaika na mradi**

**54%**

**Wanaume 26,650 walionufaika na mradi**



Kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kati ya miradi mbalimbali ambayo TEA inaifadhili katika kipindi cha mwaka 2018/2019 hadi 2022/2023, jumla ya miradi mitano yenye thamani ya shilingi bilioni 1.5 ilifadhiliwa kwenye taasisi za elimu ya juu Zanzibar.

Miradi hiyo ni pamoja na upanuzi, ujenzi na uboreshaji wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, ambayo ilitekelezwa katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Taasisi ya Utawala wa Umma (IPA).

Halikadhalika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2022/2023, TEA chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilitekeleza miradi kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF). Mfuko huo ni sehemu ya programu ya Kuendeleza Elimu ya Ujuzi na Mafunzo ya Stadi za Kazi zenye kuleta tija katika ajira (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ) na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kuendeleza Ujuzi (National Skills Development Strategy - NSDS).

Programu ya ESPJ inafadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo miradi iliyotekelezwa imenufaisha vijana 49,063, kati yao wanawake ni 22,413 sawa na asilimia 46 na wanaume 26,650, sawa na asilimia 54, kutoka maeneo mbali mbali nchini. Hii ni moja ya programu zilizotekelezwa na kuleta manufaa makubwa kwa vijana kupitia muungano.

### *Mikopo elimu ya juu*

Fursa za elimu ya juu hapa nchini zimeongezeka kupitia upatikanaji wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB). Bodi hizi zimeendelea kushirikiana katika maeneo mbalimbali kupitia muungano ambao sasa unatimiza miaka 60.

Taasisi hizi mbili ziliingia katika makubaliano rasmi ya kiutendaji kwa kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) mnamo tarehe 29 Aprili, 2021, ambapo HESLB na ZHELB pamoja na mambo mengine zimefungamanisha mifumo (systems integration) kwa lengo la kuwabaini wanafunzi walioomba mikopo na kupangiwa na bodi zote mbili ili kuepuka kutumia fedha za serikali kwa kutoa mikopo mara mbili kwa wanafunzi hao hao.

Maeneo mengine ya mafanikio katika ushirikiano huu wa kimuungano ni pamoja na kuwa na jitihada za kuwajengea uwezo watumishi na kubadilishana uzoefu, hususani katika maeneo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); utoaji mikopo na urejeshaji mikopo; kuwabaini wanufaika wa mikopo; na kukagua waajiri ili kuhimiza ufuataji wa sheria (compliance) katika urejeshaji mikopo. HESLB na ZHELB zinashirikiana katika vikao na maafisa mikopo wa vyuo vyote nchini na uelimishaji wa ana kwa ana kuhusu masuala ya mikopo ya elimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Aidha, HESLB ina ofisi kisiwani Unguja tangu mwaka 2011 na kazi hizi zinaendelea.

### *Mafunzo ya ufundi na ufundi stadi*

Hivi sasa Tanzania kupitia sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014, toleo la 2023, imetoa kipaumbele katika elimu na mafunzo ya amali, ambayo imekuwa ikiitwa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Mafunzo haya yanasimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi (NACTVET).

Kupitia muungano, baraza hili lilifungua ofisi Zanzibar mwaka 2014 ili kuimarisha ushirikiano katika utekelezaji na usimamizi wa viwango vya ubora wa mafunzo na huduma bora kwa wadau wa taasisi zinazotoa mafunzo hayo katika pande zote mbili za muungano. Kama zilivyo ofisi zingine za kanda za NACTVET, ofisi za Zanzibar zina majukumu ya kusimamia taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi kuhusu usajili; vibali na utambuzi wa idara; kuratibu na kuendesha mafunzo ya ufundishaji kwa walimu wa ufundi kuhusu matumizi ya mitaala ya uwezo; na kuhamasisha wadau kuhusu mchakato wa tathmini na uandikishaji. Hii imekuwa chachu ya kuongeza wigo wa maeneo ya mafunzo kwa maana ya vyuo na taasisi kwa vijana wa pande zote mbili za muungano.

### *Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)*

Kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1977 na kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECAT) liliingizwa katika orodha ya mambo ya muungano.

Hatua hii ilimaanisha kwamba mitihani ya taifa ya kidato cha nne na cha sita pamoja na elimu ya ualimu kwenye ngazi ya astashahada na stashahada iliingia katika masuala ya muungano na hivyo kusimamiwa na NECTA.
Kwa kuweka mitihani kwenye mambo ya muungano, Tanzania imefanikiwa kuwa na watahiniwa wenye viwango na sifa zinazolingana katika ngazi hizo za elimu.
Ni wazi kwamba muungano huu umechukua nafasi kubwa katika kuwaunganisha wananchi na kuimarisha mahusiano mazuri baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka wigo mpana kwa wananchi wake kuzitumia fursa mbalimbali zilizopo za kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa lengo la kujipatia maendeleo huku elimu ikiwa na nafasi kubwa ya kuandaa vijana wenye umahiri ili kuliinua taifa la Tanzania.
Wakati tukiadhimisha miaka 60 ya muungano, ni vyema tukatumia ipasavyo fursa zilizopo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa kuleta maendeleo yatakayoinua hali ya elimu na uchumi wa Watanzania.
Kwa hakika, ili tuzitumie vizuri fursa hizi hatuna budi tuulinde, tuuimarishe na tuudumishe muungano huu adhimu kwani ni dira ya maendeleo na mafanikio yetu.



# Jaji Warioba Ataja *Siri ya Muungano Kudumu*

Na Mawazo Kibamba, Maelezo

Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa zamani, Mhe. Jaji mstaafu Joseph Sinde Warioba, ametaja suala la Watanzania kujitambua, uhuru na usalama kama mambo ya msingi na miongoni mwa siri kubwa zinazoifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kudumu na kutimiza miaka 60 hivi leo.

Mhe. Warioba aliyasema hayo hivi karibuni nyumbani kwake jijini Dar es Salaam, wakati akifanya mahojiano maalum yaliyoratibiwa na Idara ya Habari (Maelezo), kuhusu miaka 60 ya muungano.

Mhe. Warioba alisema kuwa Watanzania wanajivunia muungano kufikisha miaka 60 kwa sababu wanajitambua wametoka wapi, wapo wapi na wapi wanakwenda; na kwamba kujitambua huko ni jambo kubwa ambalo linaufanya muungano kudumu zaidi.

Akizungumzia kuhusu suala la siri ya muungano huu kudumu ukilinganishwa na wa nchi nyingine, Mhe. Warioba alisema yapo mambo ya kujivunia katika siri hizo ambayo moja ni kujitambua; kwanza tumetoka wapi, tupo wapi na tunakwenda wapi. Alisema zaidi kuwa muungano huu ulianzishwa kukiwa hakuna hata katiba. Ni jambo kubwa sana.

Aidha, alitaja siri nyingine muhimu na ya kujivunia kwenye muungano huu kuwa ni uhuru uliopo kwa wananchi wa Tanzania ambao umewafanya kuwa huru kuishi popote pale na kufanya shughuli za kiuchumi kama kilimo ambapo mtu atapata ardhi na kulima.

"Cha kujivunia hapa ni kwamba muungano umeunganisha watu wa pande mbili za nchi; wapo huru kwa mchanganyiko wake bila shida; ni wamoja. Ningependa hata miaka 60 mingine ijayo tuendelee kuboresha na kuimarisha maisha ya wananchi wa muungano huu ili kujenga historia kwa faida ya kizazi kijacho," alieleza Mhe. Warioba.

Mhe. Warioba aliungana na Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mwingine, Mhe. John Samwel Malecela, ambapo alisema muungano huu unatakiwa kuimarishwa zaidi ili kwenda kwenye serikali moja. Hivi karibuni katika mahojiano na waandishi wa habari kuhusu miaka 60 ya muungano, Mhe. Malecela alisema hivi sasa muungano unaenda vizuri kwa kuwa na serikali mbili lakini lengo ni ni kuimarika na kuwa na serikali moja.

Mhe. Warioba alisisitiza kuhusu kuangalia mambo ambayo yanaimarisha muungano na siyo yale yanayoleta utengano na kusisitiza: "Katika kipindi hiki ambacho tunaimarisha muungano tutakuwa na serikali mbili, lakini tunakwenda kwenye serikali moja".

Aidha, alishauri muungano uboreshwe zaidi na kuongeza mambo mengi zaidi kuwa ya muungano kama vile sera za viwanda, utalii, uvuvi na uchumi wake wa buluu.

"Mwelekeo wetu uwe ni kuwaunganisha wananchi kwa kila kitu; popote anapoishi anajua anaishi Tanzania; tuache lugha ya kuonesha kwamba kuna Tanzania Bara ama Tanganyika na kuna Zanzibar. Miaka mia ijayo tutegemee Watanzania watajiona ni watu wale wale popote watakapokuwa", alieleza Mhe. Warioba wakati akihitimisha mahojiano maalum na vyombo vya habari kuhusu miaka 60 ya muungano.

# Miaka 60 ya Muungano: *TRA Ilivyoboresha Ukusanyaji wa Mapato*

Na Mawazo Kibamba, Maelezo

Miaka 60 iliyopita, Tanzania Bara na Zanzibar zilifanya uamuzi wa kihistoria kwa kuanzisha muungano, hatua iliyolenga kuunganisha nguvu za pande zote mbili kwa lengo la kujenga taifa imara na lenye mafanikio.

Katika kipindi hiki cha muda mrefu, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekuwa moja ya taasisi muhimu zinazochangia kufanikisha malengo ya muungano huu kupitia ukusanyaji wa mapato mbalimbali.

Kupitia ukusanyaji wa mapato kama kodi, tozo na ushuru, TRA imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuendesha shughuli za serikali; kuiwezesha serikali kutoa huduma za jamii kwa wananchi wake; na kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mchango wa TRA katika miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umejipambanua katika maeneo mbalimbali kama inavyoelezwa hapa chini.

### *Ukusanyaji wa Kodi kwa Kuzingatia Sheria za Kodi*

TRA imekuwa ikisimamia ipasavyo utekelezaji wa sheria za kodi na kumudu kukusanya kodi kwa njia rafiki na kuiwezesha serikali kutekeleza mipango yake ya bajeti na shughuli mbalimbali za maendeleo.

Katika miaka ya hivi karibuni TRA imeandika rekodi ya makusanyo makubwa ya kodi na kuthibitisha kuwa chombo muhimu katika ukuaji wa uchumi pamoja na kusaidia kugharamia huduma za afya, elimu, miundombinu, na maendeleo ya sekta nyingine muhimu.

Kuanzia mwaka 2021 makusanyo ya kodi yalianza kuongezeka makusanyo ya shilingi trilioni 1.4 kwa mwezi hadi shilingi trilioni 2.0 kwa mwezi. Mafanikio hayo yanatokana na mwamko mkubwa wa ulipaji kwa wafanyabiashara na mbinu bora za makusanyo.

> “Kuanzia mwaka 2021 makusanyo ya kodi yalianza kuongezeka makusanyo ya shilingi trilioni 1.4 kwa mwezi hadi shilingi trilioni 2.0 kwa mwezi.

Kuongezeka kwa makusanyo haya kunaashiria ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa shughuli za kiuchumi nchini kama vile uzalishaji viwandani, uingizaji wa bidhaa na kuimarika kwa shughuli za utalii katika kipindi cha miaka 60 ya muungano.

Aidha, ongezeko la matumizi ya mifumo ya Teknolojia na Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika usimamizi wa kodi ni hatua iliyorahisisha huduma na kukuza uhiari wa kulipa kodi, kuongezeka ufahamu na hamasa ya wananchi kuhusu masuala ya ulipaji wa kodi.

Mwezi Desemba 2023, TRA iliandika historia kubwa kwa kuvuka lengo la ukusanyaji kodi kwa asilimia 102.99 na kuweka rekodi mpya ya kiwango cha juu cha ukusanyaji wa kodi tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996.

Kiasi cha shilingi trilioni 3.05 kilikusanywa kwa mwezi Desemba, wakati lengo lilikuwa kukusanya shilingi trilioni 2.9

ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.2 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi trilioni 2.79 kilichokusanywa katika mwezi kama huo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24 (mwezi Julai mpaka Desemba 2023), TRA ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 13.92, ambayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.98 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 14.21. Makusanyo haya ya nusu mwaka ni ongezeko la asilimia 11.5 ikilinganishwa na makusanyo ya shilingi trilioni 12.49 yaliyofikiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita, 2022/23.

Mafanikio haya sasa yamechochea maboresho katika muundo wa TRA ikiwemo uanzishwaji wa divisheni mpya za walipakodi wa kati na walipakodi wadogo ili kutoa huduma bora na stahiki kwa makundi tofauti ya walipakodi, kwa kuzingatia utofauti wa mahitaji yao. Kuboreshwa kwa mazingira ya ufanyaji biashara nchini hali iliyochangia kuongezeka kwa uwekezaji, uzalishaji wa viwandani na uingizaji wa mizigo nchini.

Hali kadhalika, katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, kumekuwepo na maboresho makubwa katika mifumo ya usimamizi wa kodi za ndani na mifumo ya ukusanyaji kodi za forodha na ushuru wa bidhaa kwa upande wa Zanzibar, ikiwemo kuupa hadhi ya mkoa wa kikodi wa Pemba pamoja na ofisi za forodha zilizopo mkoani, Wesha na Wete kisiwani humo, ili kusogeza huduma karibu na wananchi, kurahisisha ulipaji kodi na kuongeza ufanisi.

TRA pia imeongeza wigo wa ukusanyaji kodi katika mitandao isiyokuwa na wakaazi kama vile Netflix, Whatsapp, Instagram, X, TikiTok, Facebook, Threads na LinkedIn.

## *Kupambana na Kudhibiti Uvujaji wa Mapato kwa Njia ya Biashara za Magendo*

TRA imekuwa ikichangia kudhibiti uvujaji wa mapato unaoweza kusababishwa na ukwepaji kodi na udanganyifu mwingine wakati wa ukusanyaji wa mapato kwa kusimamia ipasavyo sheria za kodi. Hatua hii imeongeza uaminifu katika mfumo wa kodi na kusaidia kuhakikisha kuwa serikali inapata mapato yake kikamilifu.

Kwa kufanya hivyo, serikali imeweza kupata mapato kamili yanayostahili na kuyatumia kwa njia zinazoleta manufaa kiuchumi. Uwepo wa boti za kufanya ukaguzi katika njia za magendo baharini, na udhibiti katika mipaka na viwanja vya ndege umeokoa kodi ambayo ingepotea.

Kutoa klimu ya kodi kwa Umma

Mamlaka imekuwa ikitoa elimu kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kufuata sheria za kodi kwa walipakodi na umma kwa ujumla. Hii imeongeza uelewa miongoni mwa wananchi na biashara kuhusu wajibu wao wa kodi na jinsi ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi. Kuimarishwa na kuongezeka kwa mtandao wa elimu ya kodi na utoaji wa habari kwa walipakodi na umma kwa ujumla kuhusu masuala ya kodi kama vile matumizi sahihi ya risiti za kielektroniki (EFD) na stempu za kielektroniki (ETS).

> Mapato yanayokusanywa na TRA huongeza pato la wastani la wananchi na kuchochea matumizi ya ndani.

Kampeni maalumu za kuwatembelea walipakodi katika maeneo yao ya biashara yaani “Mlango kwa Mlango” imekuwa kichocheo kikubwa cha elimu kwa mlipa kodi, elimu kwa umma na kampeni mbalimbali za elimu kwa wananchi na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kufuata sheria za kodi, imeongeza uelewa miongoni mwa jamii kuhusu wajibu wao wa kodi na jinsi ya kushiriki katika maendeleo ya nchi kwa njia ya ukusanyaji wa mapato.

## *Kuwezesha Maendeleo ya Sekta ya Biashara*

TRA inasaidia mazingira bora ya biashara kwa kusimamia sheria za kodi na kutoa huduma za ushauri kwa wafanyabiashara na hivyo kuchochea uwekezaji na kukuza sekta binafsi, ambayo ni injini muhimu ya ukuaji wa uchumi.

## *Kugharamia Miradi ya Maendeleo*

Kupitia mapato inayokusanya, TRA imekuwa ikichangia pia katika ujenzi na uimarishaji wa miundombinu muhimu kama vile barabara, reli, bandari, na viwanja vya ndege. Hii imesaidia kuboresha mifumo ya usafirishaji na kuchochea biashara na shughuli za kiuchumi huku ikiwezesha upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi.

## *Kuwezesha Uwekezaji*

Serikali inapokuwa na uwezo wa kutosha wa kugharamia miradi ya maendeleo, inavutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi. Hii huleta mitaji mipya, teknolojia, na ujuzi ambao husaidia kuongeza uzalishaji, kukuza ajira, na kuongeza thamani katika sekta mbalimbali za uchumi.

## *Kuongeza Matumizi ya Ndani*

Mapato yanayokusanywa na TRA huongeza pato la wastani la wananchi na kuchochea matumizi ya ndani. Hii husaidia kukuza biashara ndogo na za kati, kuzalisha mahitaji zaidi ya bidhaa na huduma, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

## *Kuwezesha Ushindani wa Kimataifa*

Kupitia mapato yanayokusanywa, serikali imeweza kuwekeza katika kuimarisha sekta muhimu za uchumi na kuongeza ushindani wa nchi katika soko la kimataifa. Hii ni pamoja na kuwekeza katika utafiti na maendeleo, elimu na mafunzo ya kitaalam, na kukuza sekta za kilimo, viwanda, na huduma.

TRA pia inatumia mifumo ya kielektroniki kufuatilia mizigo inayopita katika bandari kuu nchini na kusafirishwa kwenda nchi jirani. Mifumo hiyo ni ile ya TANCIS na ECTS inayoiwezesha TRA kufuatilia mzigo huo ili usishushwe ndani ya nchi kwa kuhakikisha unatoka nje ya nchi na kupelekwa kwenye nchi husika kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Zambia, Burundi au Rwanda. Mifumo hii inaongeza ufanisi na uaminifu kwa nchi zinazoagiza mizigo yake kupitia Tanzania.



Kwa kuzingatia mambo haya, ni wazi kuwa ukusanyaji wa mapato unaofanywa na TRA umekuwa msingi muhimu wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania na Zanzibar katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kudumisha juhudi hizi na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha kuwa faida za maendeleo zinawanufaisha wananchi wote na kusaidia kuleta maendeleo endelevu.

Katika miaka 60 ya Muungano, mifumo ya kielektroniki iliyotumiwa na TRA, imekuwa mhimili muhimu wa kuimarisha ukusanyaji mapato; hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Utekelezaji wa teknolojia ya kielektroniki katika shughuli za ukusanyaji kodi na usimamizi wa mapato umewezesha ufanisi mkubwa, uwazi, na udhibiti bora wa mchakato mzima. Hapa chini ni baadhi ya njia ambazo mifumo ya kielektroniki imechangia katika kukuza ukusanyaji wa mapato katika kipindi hicho.

### *Urahisi wa Malipo*

Kuanzishwa kwa njia za malipo ya kielektroniki kama vile malipo kupitia mtandao, simu za mkononi, au kadi za benki kumefanya iwe rahisi kwa walipakodi kulipa kodi zao. Hii inapunguza urasimu, kupunguza fursa za rushwa, na kuongeza ufanisi katika mchakato mzima wa malipo.

### *Uwezeshaji wa Huduma za Mtandaoni*

TRA imeanzisha huduma za mtandaoni kama vile usajili wa kodi, uwasilishaji wa taarifa za kodi, na kupata taarifa za malipo. Huduma hii imefanya iwe rahisi kwa walipakodi kutekeleza majukumu yao ya kodi na kuongeza uwazi katika mchakato wa ukusanyaji wa mapato.

### *Uwekezaji katika Ufundi na Mafunzo*


TRA imekuwa ikifanya uwekezaji mkubwa ili kuhakikisha wafanyakazi wake wanapata mafunzo na ujuzi unaohitajika katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki. Uamuzi huu umeleta ufanisi na kuongeza uwezo wa kuchambua na kutumia taarifa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.
Kwa ujumla, mifumo ya kielektroniki ndani ya TRA imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza ukusanyaji wa mapato na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania na Zanzibar kuelekea kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya muungano.

Mafanikio makubwa ya ukusanyaji wa kodi ni matokeo ya kuimarika kwa matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi, mazingira ya ufanyaji biashara nchini na mwenendo wa ulipaji wa kodi kwa hiari katika kipindi cha miaka 60 ya muungano.

Aidha, utatuzi wa migogoro ya kodi nje ya mahakama na kuongezeka kwa kiwango cha uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa mlipakodi kwa njia mbalimbali nako kumechangia katika kuboresha utendaji wa TRA.
Ni hakika kwamba katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, TRA imeonesha umuhimu wake katika kuiendeleza nchi kupitia ukusanyaji mapato, udhibiti wa uvujaji wa mapato, elimu kwa umma, na kuimarisha mazingira ya biashara. TRA imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa wananchi wa Tanzania na Zanzibar licha ya kuwa bado kuna changamoto.
Mwisho.



# Mafanikio Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa katika *Miaka 60 ya Muungano*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mmwenyekiti wa kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, Prof. Rwekaza Mukandala, aliyeambatana na baadhi ya wajumbe wa kikosi kazi hicho Ikulu, jijini Dar es Salaam, tarehe 30 Mei, 2022.*

Na Mwandishi Wetu, ORPP

Miaka 60 imetimia tangu Tanganyika na Zanzibar zilipoungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 26 Aprili, 1964.

Baada ya muungano huo, taasisi mbalimbali zimeundwa kwa nyakati tofauti ili kuiendeleza Tanzania katika nyanja za kiuchumi, kijamii, na kisiasa.

Moja ya taasisi hizo ni Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (ORPP) iliyoanzishwa mwaka 1992, ili kuhakikisha uwepo na ukuaji wa demokrasia ya vyama vingi nchini.

Tunapojivunia miaka 60 ya muungano, hatuna budi kuangalia mafanikio yaliyopatikana katika ofisi hii yenye umuhimu mkubwa nchini Tanzania.

Hadi kufikia 2024, ofisi hii imeongozwa na viongozi wafuatao: Mhe. Jaji George Bakari Liundi (1992-2001), Mhe. John Billy Tendwa (2001-2013), Mhe. Jaji Francis S. K. Mutungi (2013 hadi sasa). Viongozi hawa wamepata usaidizi adhimu kutoka kwa manaibu wao ambao ni Mhe. Abdulwahid Masoud Borafia (1992-1993), Mhe. Rajabu Baraka Juma (2004-2017), Mhe. Mohammed Ally Ahmed (2018 hadi sasa).

Majukumu ya ofisi hii ni kusajili vyama vya siasa na kuvifuta vilivyokiuka masharti ya usajili kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya mwaka 1992; kuratibu shughuli za Baraza la Vyama vya Siasa, na kufuatilia mapato na matumizi ya vyama vya siasa katika uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010.

Mengine ni kufuatilia utendaji wa vyama vya siasa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992, kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa vyenye sifa, kuwa kiungo kati ya Serikali na Vyama vya Siasa nchini, na kutoa elimu kwa umma kwa vyama vya siasa na wadau wa vyama vya siasa.

Hadi kufikia Februari 2024, Tanzania ina jumla ya vyama vya siasa 19 vilivyosajiliwa na ofisi hii. Vyama hivyo ni Chama cha Mapinduzi (CCM), The Civic United Front (CUF), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Union for Multiparty Democracy (UMD), National Convention for Construction and Reform (NCCR-Mageuzi), National League for Democracy (NLD), na United Peoples' Democratic Party (UPDP).

Vingine ni National Reconstruction Alliance (NRA), African Democratic Alliance Party (ADA-TADEA), Tanzania Labour Party (TLP), United Democratic Party (UDP), Chama cha Demokrasia Makini (MAKINI), Democratic Party (DP), Sauti ya Umma (SAU), Alliance for African Farmers Party (AAFP), Chama cha Kijamii (CCK), Alliance for Democratic Change (ADC), Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), na Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo).

Pamoja na hilo, ofisi imefanikiwa kufuatilia mienendo ya vyama vya siasa ili kuhakikisha vyama hivyo vinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Gharama za Uchaguzi na sheria za nchi.

Aidha, ORPP imefanikiwa kufuatilia utendaji kazi wa vyama vya siasa na kugawa ruzuku ya kila mwezi kwa vyama vya siasa vyenye sifa kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Vyama vya Siasa, Na. 5 ya mwaka 1992, ambapo vyama vya siasa vilivyopata angalau asilimia tano ya kura zote halali zilizopigwa katika uchaguzi mkuu na vyama vyenye wabunge au madiwani, vimekuwa vikipata ruzuku hiyo.

Sambamba na hayo, ORPP imefanikiwa kuwa kiungo kati ya serikali na vyama vya siasa nchini huku ikiendelea kutoa elimu kwa umma, vyama vya siasa na wadau wa vyama vya siasa.

Tukiwa tunaadhimisha muungano wetu, tunapaswa kukumbusha kazi kubwa iliyofanywa na ofisi hii chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye aliunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini kilichofanya kazi ya kuchambua maoni ya wadau kwa kipindi cha miezi 10.

"Katika shukrani nisiisahau Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, wakiongozwa na Jaji Mutungi; Jaji Mutungi saa zingine ananipigia simu usiku we Mama wee hii kazi uliyonipa nimekwama hapa na hapa. umeaminiwa kuwa Msajili wa Vyama vya Siasa nenda na kazi yako, ukikwama fedha niambie, lakini mengine fanya kazi yako. Kwa hiyo nakushukuru umefanya kazi yako na mmefikia pazuri," alisema Mhe. Rais Samia akiwa katika moja ya matukio ya kitaifa.

ORPP imeiwezesha Tanzania kuwa na vyama vya siasa imara ambavyo vitahamasisha ukuaji na kudumisha demokrasia ya vyama vingi nchini.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatambua mchango wa marais wa awamu zote katika kukuza demokrasia nchini. Rais Julius Nyerere alishinikiza kuasisiwa kwa demokrasia ya vyama vingi huku Rais Ali Hassan Mwinyi akisimamia ujenzi wa demokrasia ya vyama vingi na uhuru wa vyombo vya habari.

Katika mtiririko huo, Rais Benjamin Mkapa aliimarisha vipengele muhimu vya demokrasia vya uwazi na utawala bora huku Rais Jakaya Kikwete akijikita katika kuimarisha haki za binadamu, uhuru wa vyombo vya habari, na uhuru wa kujieleza.

Hapa karibuni Rais John Magufuli aliasisi uwajibikaji wa kidemokrasia katika utoaji wa huduma za umma ambapo wananchi walipewa nafasi ya kudai uwajibikaji wa maafisa wa serikali na kushuhudia demokrasia ikiimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hivi sasa Rais Samia Suluhu Hassan akijikita kwenye uhuru wa kujieleza na uhuru wa maoni, uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kuandamana, uhuru wa mikutano ya vyama vya siasa, na haki za binadamu.

*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akifungua mkutano maalum wa Baraza la Vyama Vya Siasa, tarehe 11 Septemba, 2023, jijini Dar es Salaam.*



# *Miaka 60 ya Muungano* na Ongezeko la Majaji Mahakama ya Rufani Tanzania

Mahakama ya Rufani ndiyo Mahakama ya juu kuliko zote nchini Tanzania ambayo ilianzishwa chini ya Ibara ya 117 (1) ya Katiba ya Tanzania, 1977.

Na Mwandishi Wetu, Mahakama ya Tanzania

Kwa mujibu wa Ibara ya 4(2) na 107A(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chombo chenye mamlaka na kauli ya mwisho katika kutekeleza utoaji haki ni Mahakama ya Tanzania inayojumuisha Mahakama ya Rufani, ambayo hutoa huduma kwa pande zote za muungano. Mahakama ya Rufani ndiyo Mahakama ya juu kuliko zote nchini Tanzania ambayo ilianzishwa chini ya Ibara ya 117 (1) ya Katiba ya Tanzania, 1977. Jaji Mkuu ambaye huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Mahakama ya Rufani.

Katika shughuli za kila siku za Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu husaidiwa na Msajili wa Mahakama ya Rufani, kama Mkuu wa Masijala ya Mahakama; Naibu Msajili Mwandamizi na Naibu Wasajili wa Mahakama hiyo. Msajili wa Mahakama ya Rufani husimamia utendaji wa kazi za Mahakama, kuratibu pamoja na kuwasiliana na Jaji Mkuu kuhusu masuala yanayohusu shughuli za kila siku za Mahakama.
Kwa mujibu wa muundo mpya wa Mahakama, usimamizi wa kila siku wa shughuli za kiutawala na uendeshaji wa Mahakama kwa Mahakama ya Rufani husimamiwa na Mtendaji wa Mahakama ya Rufani.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma mara baada ya kuwasili katika Viwanja vya Chinangali kwa ajili ya kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Sheria nchini ambayo Kitaifa yamefanyika Jijini Dodoma tarehe 01 Februari, 2024.

### *Historia ya Mahakama ya Rufani*

Mwaka 1963 mfumo mpya ulianzishwa ambao uliunganisha mahakama za wenyeji na Mahakama Kuu na kuondoa ubaguzi wa rangi na ukatenganisha mahakama na utawala wa kiserikali. Sheria za kimila zilitambuliwa na kuunganishwa ili kuondoa migongano ya sheria.

Mabadiliko ya mwaka 1963 yaliweka msingi wa mfumo wa mahakama zilizo chini ya Mahakama Kuu ambao ndio upo hadi sasa.

Katika kipindi hicho rufaa kutoa Mahakama Kuu zilipekwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki (EACA) na jaji mkuu wa kwanza Mtanzania aliyeongoza Mahakama Kuu ya Tanzania alikuwa Mhe. Augustino Saidi, ambaye alihudumu kuanzia mwaka 1971 hadi mwaka 1977.

Rufaa za kutoka Mahakama Kuu ziliendelea kupelekwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki hadi mwaka 1979 ilipoanzishwa Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Mahakama ya Rufani ilianza na majaji wa rufani watano ikimjumuisha na jaji mkuu na wakifanya kazi katika masijala ya Dar es Salaam. Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilianzishwa kwa Sheria Namba 15 ya mwaka 1979 iliyoanza kutumika tarehe 9 Agosti 1979. Mahakama ya Rufani ilianza kufanya kazi baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mnamo tarehe 22 Oktoba 1979.
Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1977 kulizilazimisha nchi wanachama, Tanzania, Kenya na Uganda, kuanzisha mahakama zao za rufani ili kuchukua nafasi ya Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki.

Mabadiliko ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sheria Na. 14 ya mwaka 1979) yaliianzisha rasmi Mahakama ya Rufani ya Tanzania chini ya Ibara ya 68A ya zamani ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 ambayo sasa ni Ibara ya 117(1).

Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilichukua nafasi ya Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki iliyoanzishwa chini ya Ibara ya 80 ya Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa mwaka 1967. Bunge la Tanzania lilitunga Sheria ya Mamlaka ya Rufaa ya mwaka 1979 ili kuweka taratibu za rufaa kushughulikiwa na Mahakama ya Rufani ya Tanzania iliyokuwa imeanzishwa.

Kati ya mwaka 1977 na tarehe 9 Agosti, 1979, kulikuwa na Mahakama ya Rufani ya "muda" ya Afrika Mashariki ndani ya Tanzania iliyoongozwa na Jaji Abdullah Mustafa, kama Kaimu Rais. Majaji wengine waliazimwa kutoka Mahakama Kuu kwa muda. Uteuzi wa muda wa Jaji Mustafa kuwa Kaimu Rais wa Mahakama ya "muda" ulimalizika wakati Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilipoanzishwa na kuzinduliwa tarehe 22 Oktoba, 1979.

Tangu kuanzishwa kwake, Mahakama ya Rufani imeshaongozwa na Mhe. Jaji Francis Lucas Nyalali kuanzia mwaka 1977 hadi 2000; Mhe. Jaji Barnabas Albert Samatta kutoka mwaka 2000 hadi 2007; Mhe. Jaji Augustino Ramadhan kutoka mwaka 2007 hadi 2011; Mhe. Jaji Othman Chande kutoka mwaka 2011 hadi 2017; na Mhe. Jaji Prof. Ibrahim Hamis Juma kutoka 2017 hadi sasa.

Wakati ilipoanzishwa tarehe 22 Oktoba, 1979, Mahakama ya Rufani ilikuwa na masijala moja tu jijini Dar es Salaam. Baadaye Mahakama ilianzisha masijala ndogo katika kanda za Mwanza na Arusha ili kurahisisha huduma kwa wananchi waliokuwa wakisafiri umbali mrefu kuja Dar es Salaam kufungua rufaa zao.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akipokea zawadi ya picha ya Majaji Wakuu wa Nchi za Kusini na Mashariki Mwa Afrika kutoka kwa mwenyekiti wa jukwaa hilo ambaye pia ni Jaji Mkuu wa Namibia, Mhe. Peter Shivute, wakati wa mkutano huo uliofanyika katika hoteli ya Mount Meru, Jijini Arusha tarehe 23 Oktoba, 20,23.



### *Mamlaka ya Mahakama ya Rufani*

Mahakama ya Rufani inapata mamlaka yake kutoka katika katiba na sheria zilizotungwa na Bunge. Sheria ya Mamlaka ya Rufaa ya mwaka 1979 ilitoa mamlaka kwa mahakama ya rufani za mahakama kuu za Tanzania na Zanzibar.

Vituo vya usikilizaji wa mashauri ya Mahakama ya Rufani viko katika masijala za Mahakama Kuu za Arusha, Dar es Salaam, Bukoba, Dodoma, Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Moshi, Musoma, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Songea, Sumbawanga, Tabora, Tanga na Zanzibar.

Katika kusikiliza rufaa, majaji watatu wanaunda mahakama kamili na uamuzi wa mahakama ni wa walio wengi. Katika matukio mengine, majaji watano au majaji saba wanaweza kuunda mahakama kutegemeana na shauri husika linalosikilizwa. Jaji mmoja anaweza kukaa katika chumba chake kusikiliza maombi ambayo yanastahili kuamuliwa na jaji mmoja.

### *Miaka 60 ya muungano katika Mahakama ya Rufani*

Wakati Tanzania ikiadhimisha miaka 60 ya muungano wake kumekuwepo na ongezeko la majaji wa rufani. Ongezeko la majaji wa Mahakama ya Rufani limeenda sambamba na uanzishwaji wa masijala ndogo ya Mahakama ya Rufani.

Wakati Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiingia madarakani mwezi Machi 2021, kulikuwa na majaji wa rufani 16; na katika uongozi wake hadi kufikia tarehe 3 Septemba, 2023, idadi ya majaji wa rufani imeongezeka na kufikia 35 ikiwa ni zaidi ya ongezeko la asilimia 100.
Ongezeko la majaji wa Mahakama ya Rufani kwa sasa linawezesha majopo 11 ya majaji watatu; majopo saba ya majaji watano; na majopo matano ya majaji saba kuendesha vikao vya Mahakama ya Rufani kwa wakati mmoja. Idadi ya vituo vya kusikilizia mashauri ya Mahakama ya Rufani imeongezeka kutoka 16 wakati Rais Samia akiingia madarakani na kufikia vituo 18 mpaka sasa.
Vituo vya usikilizaji wa mashauri ya Mahakama ya Rufani viko katika masijala za Mahakama Kuu za Arusha, Dar es Salaam, Bukoba, Dodoma, Iringa, Kigoma, Mbeya, Morogoro, Moshi, Musoma, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Songea, Sumbawanga, Tabora, Tanga na Zanzibar.
Kumekuwepo na faida zilizotokana na kuongezeka kwa majaji wa mahakama ya rufani ikiwa ni pamoja na kupunguza mrundikano wa mashauri, kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi katika masijala zote za Mahakama Kuu; mashauri kusajiliwa na kuamuliwa kwa wakati na kupunguza mzigo kwa majopo yaliyokuwepo.
Ujenzi wa kituo jumuishi cha utoaji haki Pemba, ambao utaanza hivi karibuni ni miongoni mwa mafanikio yanayolenga kusongeza huduma za utoaji haki karibu na wananchi. Uwepo wa kituo hicho utaiwezesha Mahakama ya Rufani kuwa na masijala yake ndogo, hivyo kuongeza idadi ya vikao vya mahakama kwa upande wa Zanzibar.



# Mafanikio ya Bunge la Tanzania katika *Miaka 60 ya Muungano*

**Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilianzishwa mwaka 1964 likiwa miongoni mwa vyombo vyenye mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya muungano wa Tanganyika na Zanziabar.**

Na Mwandishi Wetu

Miaka 60 ni umri wa mtu mzima ambaye anaweza kuwa na wajukuu na pengine watu wanaanza kumwita mzee. Miaka hiyo pia yaweza kuwa ishara ya mtumishi wa umma kumaliza utumishi wake baada ya miaka mingi. Hali kadhalika, miaka hiyo inampa mtu heshima ya kuaminika kuwa na uzoefu, ujuzi, hekima, busara na hadhi ya kipekee katika jamii.

Maelezo hayo ni sawa na umri ulivyo wa muungano wa Tanzania wa miaka 60. Umri huo umekuwa ni safari ndefu inayojumuisha kupiga hatua za mafanikio ya kimaendeleo kwa nchi na mihimili yake ya utawala likiwemo Bunge.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilianzishwa mwaka 1964 likiwa miongoni mwa vyombo vyenye mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya muungano wa Tanganyika na Zanziabar. Chimbuko lake linatokana na Hati ya Makubaliano ya Muungano iliyosainiwa Zanzibar mnamo tarehe 22 Aprili, 1964.

Mambo yaliyosukuma muungano huo ni pamoja na mahusiano ya karibu ya kisiasa, urafiki, udugu wa damu, lugha ya pamoja ya mawasiliano, yaani Kiswahili, na shughuli za pamoja za kiuchumi kama vile uvuvi, kilimo na biashara.

Upekee wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa wa kipekee duniani kwani ulifikiwa kwa makubaliano ya hiari baina ya wananchi wa nchi mbili huru na sasa umedumu kwa zaidi ya nusu karne. Miungano mingine duniani kama ya Marekani, Uingereza au Imarata (UAE), haikufikiwa kwa njia hii bali mazingira tofauti.

Kudumu kwa muungano huu ni kiini cha maendeleo ya uhai wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, mambo yote yanayofanikisha kudumu na kushamiri kwa muungano huu ni sababu halisi za kuendelea kuwepo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.





Bw. Adam Sapi Mkwawa, Spika wa kwanza wa Bunge huru la Tanganyika wakati Tanganyika ikipata uhuru wake kutoka kwa waingereza mwaka 1961.

Mafanikio ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliyoanza kuonekana tangu awali wakati wa kusaini Hati za Makubalino ya Muungano, yanachangia kuimarika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na pia yanatokana na mchango wa bunge hilo. Tarehe 26 Aprili, 1964, Mkataba wa Muungano ambao ni chimbuko la Bunge la Jamhuri ya Muungano ulithibitishwa na kukubaliwa na vyombo vya kutunga sheria vya pande zote mbili, yaani Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

Hatua hiyo ilikuwa ishara ya muungano ulioambatana na kuanzishwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano kukubalika na wananchi wa pande zote mbili. Hatua hiyo ilionesha dalili njema ya mustakabali wa muungano, na matokeo yake imetimia miaka 60 iliyojaa mafanikio mbalimbali yakiwemo yanayohusu chombo cha uwakilishi wa wananchi kinachoitwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuzungumzia mafanikio ya miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar bila kugusa taasisi muhimu kama mhimili wa bunge si jambo linalowezekana. Bunge ni chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria za mambo yote ya muungano na yasiyo ya muungano yanayohusu Tanzania Bara. Kadhalika, bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi kutoka pande zote za muungano.

Kutokana na muungano, bunge hili limepitia hatua mbalimbali za mafanikio tangu kuanzishwa kwake. Bunge hili liliundwa na wajumbe wa kutoka Bunge la Tanganyika na wengine kutoka Baraza la Mapinduzi Zanzibar kama wabunge wake wa kwanza. Mafanikio hayo yamejidhihirisha katika nyanja mbalimbali, mathalani: kutungwa kwa sheria mbalimbali za muungano; kukua kwa nafasi ya uwakilishi wa wananchi wa pande zote za muungano bungeni; kuimarika kwa ushirikiano na mahusiano ya bunge kimataifa; kuimarisha nafasi ya wanawake kwenye vyombo vya maamuzi; kuongeza usimamizi wa utekelezaji wa majukumu ya serikali kwa uwazi na uwajibikaji; na kuboresha miundombinu ya bunge. Aidha, majukumu ya bunge ambayo ni kuisimamia na kuishauri serikali, yamewezesha utekelezaji mzuri wa mipango mbalimbali iliyoleta maendeleo Tanzania. Kwa ujumla, bunge limekuwa sehemu ya mafanikio yote ya serikali kwa kuwa mipango na bajeti zote za serikali zinapata kibali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muunganbo wa Tanzania.
Maeneo mengine ambayo bunge limefanikiwa katika kipindi cha miaka 60 ya muungano ni pamoja na: kudumisha utawala bora, kupata nafasi za juu za uongozi wa kibunge kimataifa, kuongezeka kwa wageni wanaolitembelea bunge hili wakiwamo wakuu wa nchi mbalimbali na kuimarisha michezo mbalimbali kwa wabunge.

Mafanikio ya miaka 60 ya muungano kupitia bunge hili katika nyanja mbalimbali zilizotajwa yanaelezwa kwa undani zaidi katika aya zifuatazo: -

### *Kutungwa sheria mbalimbali*

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliwezesha kuanzishwa kwa bunge la pamoja liitwalo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo limedumu tangu kuasisiwa kwa muungano mwaka 1964 likitekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwawakilisha wananchi wa pande zote mbili katika utungaji sheria za nchi na usimamiaji wa shughuli za umma. Vilevile, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeendelea kuzingatia maslahi ya wananchi wa pande zote mbili za muungano kwa kuchambua, kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya kila mwaka kwa amani, uelewano na weledi.

Katika kutekeleza majukumu yake, miongoni mwa sheria zilizotungwa na Bunge katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, zipo zinazohusu masuala ya fedha, ushuru wa forodha na bidhaa, posta na simu, takwimu, usajili wa vyama vya siasa, mambo ya ndani ya nchi, ulinzi, mambo ya nje, maaliasili, elimu ya juu, utabiri wa hali ya hewa, usafiri na usafirishaji wa anga, utumishi wa umma katika Serikali ya Muungano, Baraza la Taifa la Mitihani, Mahakama ya Rufani na mambo mengine yote yaliyoanishwa katika Nyongeza ya Kwanza iliyotajwa katika Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### *Kukua kwa nafasi ya uwakilishi wa wananchi bungeni*

Miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni kipindi ambacho ongezeko la nafasi ya uwakilishi wa wananchi katika chombo cha kutunga sheria limeshuhudiwa. Mabadiliko mbalimbali ya mara kwa mara ya idadi ya wabunge kutoka pande zote za muungano kulingana na ongezeko la watu na ukuaji wa miji yamejitokeza. Mwaka 1964 Bunge la Tanganyika na Zanzibar lilikuwa na wabunge 98, ambapo kwa nyakati tofauti idadi hiyo imekuwa ikiongezeka hadi kufikia wabunge 393 waliopo sasa. Idadi hiyo ni sawa ana ongezeko la asilimia 301 kwa miaka 60 ya muungano.

Kwa upande wa uwakilishi wa wabunge wa Zanzibar kwenye bunge la Muungano, mwaka 1965 idadi yao ilikuwa 35 kati ya wabunge 183 wa bunge hilo, sawa na asilimia 19. Leo miaka 60 ya muungano inapotimia, idadi ya wabunge wa Zanzibar ndani ya bunge la muungano ni 78 kati ya 393, sawa na asilimia 20, yaani kila idadi ya jumla inapoongezeka na idadi ya wabunge wa Zanzibar nayo pia inaongezeka.

## *Kuimarisha nafasi ya wanawake kwenye vyombo vya uamuzi*

Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuongeza idadi ya uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za mamlaka na ushiriki kwenye vyombo vya uamuzi. Bunge limekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza Tamko la 181 la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu ambalo linatambua kuwa kila mtu ana haki ya kushiriki katika maamuzi ya serikali ama nchi yake.

Aidha, bunge linaheshimu maazimio ya Mkutano wa Beijing na Itifaki za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yanayohimiza usawa kwa wote na kuhakikisha nchi wanachama zinafikisha angalau asilimia 30 ya nafasi za maamuzi kwa wanawake. Hatua hizo za bunge zinadhihirika kwa kuangalia yafuatayo:

## *Idadi ya Wabunge Wanawake*

Ibara ya 66(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeweka masharti ya bunge kuwa na viti maalum vya wabunge wanawake wasiopungua asilimia 30 ya wabunge wote. Sharti hili linalenga kuhakikisha kuwa kwa namna yoyote ile, idadi ya wabunge wanawake haipungui asilimia 30 tofauti na masharti yaliyokuwepo kabla ya muungano.

Aidha, pamoja na ulazima wa viti maalum vya wabunge wanawake uliowekwa na katiba, bunge limeendelea kuongeza idadi ya wabunge wanawake kupitia majimbo, kuteuliwa na rais, na nafasi ya wabunge kutoka Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Mwaka 1964, bunge la muungano lilipoanza, idadi ya wabunge wanawake ilikuwa saba kati ya wabunge 98, sawa na asilimia 7.14. Idadi ya wabunge wanawake katika miaka 60 ya muungano imeongezeka hadi kufikia wabunge wanawake 147 hivi sasa, sawa na asilimia 37.4 ya wabunge wote.

## *Wanawake katika Nafasi za Uongozi wa Bunge*

Ongezeko la wabunge wanawake haliishii kwenye nafasi za uwakilishi pekee bali pia katika nafasi za uamuzi bungeni. Idadi hiyo iligusa nafasi mbalimbali za uongozi wa bunge ambazo ni pamoja na nafasi ya Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti wa Bunge, Kiongozi wa Upinzani na Katibu wa Bunge na bila kusahau nafasi ya Mkuu wa Nchi, yaani Rais, ambaye kwa mujibu wa Ibara ya 62(1) na 63(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni sehemu ya bunge.

## *Rais wa Nchi akiwa Sehemu ya Bunge*

Ibara ya 62(1) na 63(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeweka bayana kwamba bunge linaundwa na sehemu mbili: sehemu moja ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na sehemu ya pili ni wabunge. Tangu kuundwa kwa muungano wa Tanzania, sehemu ya kwanza ya bunge ambayo ni rais wa nchi imekuwa ikishikiliwa na viongozi wanaume, hadi mwezi Machi 2021 alipoingia Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, rais wa sasa wa Tanzania ameweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa sehemu ya bunge katika nafasi yake ya Mkuu wa Nchi.

## *Spika na Naibu Spika wa Bunge*

Kwa nafasi ya Naibu Spika wa Bunge, Mhe. Anne Semamba Makinda alikuwa mwanamke wa kwanza kuishika mwaka 2005 na baadaye akachaguliwa kuwa Spika, akiwa pia mwanamke wa kwanza mwaka 2010. Vivyo hivyo, Mhe. Dkt. Tulia Ackson akawa mwanamke wa pili katika historia kuwa Naibu Spika mwaka 2015 na kisha Spika wa Bunge mwaka 2022.

## *Wenyeviti wa Bunge*

Kwenye nafasi ya wenyeviti wa bunge, mwananke wa kwanza alikuwa ni Mhe. Anne Semamba Makinda. Aidha, mabadiliko ya Kanuni za Bunge ya mwaka 2007 yaliweka sharti la uwakilishi wa jinsi na pande mbili za muungano. Bunge likaendelea kuwachagua wenyevikiti wanawake akiwemo Mhe. Jenista Mhagama, Mhe. Mary Mwanjelwa, na Mhe. Najma Murtaza Giga ambaye ndiye Mwenyekiti wa Bunge hadi sasa.

Baadhi

ya kamati za kudumu za bunge zimekuwa zikiongozwa na wabunge wanawake kwa nafasi ya mwenyekiti na makamu mwenyekiti. Kamati za Usimamizi wa Fedha ikiwemo Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) nazo zimeshawahi kupata wenyeviti wanawake. Mwanamke wa kwanza kuwa mwenyekiti wa kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma ni Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa PAC mwaka 2016. Kwa upande wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, mwanamke wa kwanza kuwa mwenyekiti alikuwa Mhe. Grace Tendega. Kwa sasa, jumla ya kamati tano kati ya 19 zinaongozwa na wenyeviti wanawake. Aidha, kamati sita zina makamu wenyeviti wanawake.

### *Kiongozi wa Upinzani Bungeni*

Kwa upande wa nafasi ya kiongozi wa kambi rasmi ya upinzani bungeni ambayo kwa sasa inajulikana kama Kambi Rasmi ya Walio Wachache, kwa mara ya kwanza iliongozwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni aliyekuwa mbunge mwanamke. Mbunge huyo aliyeongoza jimbo la Chake Chake, Pemba, mwaka 1995 hadi 2000, alikuwa Mhe. Fatuma Mussa Maghimbi.

### *Katibu wa Bunge*

Kwa nafasi ya Katibu wa Bunge ambayo ni ya kuteuliwa na Rais, imekuwa ikishikiliwa na wanaume tangu kuanzishwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, mwaka 2021, Rais wa Jamhuri ya Muunago wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alibadilisha historia kwa kumteua Bi. Nenelwa Mwihambi, kuwa Katibu wa Bunge; hivyo kuwa mwanamke wa kwanza katika nafasi hiyo ambayo bado anaendelea nayo.

### *Viongozi wa Kibunge katika Ngazi za Kimataifa*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekuwa na mafanikio makubwa ya kupata viongozi mahiri waliotokana na bunge hilo kuchaguliwa kuongoza taasisi mbalimbali za kibunge kimataifa. Miongoni mwa wabunge hao ni: Mhe. Getrude Ibengwe Mongella aliyechaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika mwaka 2004 hadi 2009; Mhe. Dkt. William Ferdnand Shija ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA) mwaka 2007 hadi 2014; Mhe. Dkt. Tulia Ackson, aliyechaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) mwaka 2023, nafasi anayoitumikia hadi sasa; na Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc, ambaye amekuwa Katibu wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika tangu mwaka 2021 hadi sasa.

### *Makao Makuu ya Vyama vya Kibunge*

Miongoni mwa mafanikio ya kujivunia katika miaka 60 ya muungano ni pamoja na Tanzania kuwa mwenyeji wa makao makuu ya vyama vya kibunge ikiwa ni pamoja na makao makuu ya Chama cha Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (CPA) - Kanda ya Afrika, yaliyopo bungeni Dodoma tangu mwaka 2003; na makao makuu ya Bunge la Afrika Mashariki yaliyopo Arusha tangu mwaka 2001. Mafaniko haya ni ishara ya kuwepo kwa amani, utulivu na mazingira rafiki kwa shughuli za kimataifa hapa Tanzania.

Kuwepo kwa makao makuu ya CPA Afrika kumevutia uwekezaji wa hoteli ya kisasa ya kitalii ya hadhi ya nyota 5 itakayokuwa sehemu ya vitega uchumi vya chama hicho cha kibunge. Hoteli hiyo inatarajiwa kujengwa jijini Dodoma.

### *Ushirikiano na Mahusiano ya Bunge Kimataifa*

Bunge linajivunia mafanikio ya kuwa mwanachama wa vyama mbalimbali vya kibunge vya kikanda na kimataifa ambavyo vimeongeza uzoefu wa wabunge wa Tanzania katika uendeshaji bora wa shughuli za bunge; kujenga ushirikiano; kudumisha utawala bora; na kukuza diplomasia ya kibunge kimataifa. Miongoni mwa vyama vya kibunge ambavyo bunge la Tanzania ni mwanchama ni pamoja na Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-PF), Bunge la Afrika (PAP), Bunge la Nchi Wanchama wa Jumuiya ya Madola (CPA), Bunge la Pamoja la Nchi za Umoja wa Ulaya, Afrika, Karibe na Pasifiki, (ACP/EU JA), Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Kimataifa ya Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR), na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU).

Mbali na vyama hivyo, bunge la Tanzania linajivunia pia kuwa na mahusiano na nchi mbalimbali kupitia vyama vya urafiki wa kibunge ulioanzishwa kwa Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mabunge ya nchi mbalimbali duniani.

### *Uenyeji wa Mikutano Mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa*

Eneo lingine la mafanikio ya bunge hili la muungano ni kuwa mwenyeji mikutano mbalimbali ya kimataifa ya kibunge kama vile Mkutano wa 50 Chama cha Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola uliofanyika Zanzibar tarehe 30 Agosti hadi 5 Septemba, 2019; na Mkutano wa 53 wa SADC-PF uliofanyika tarehe 2–8 Julai, 2023, jijini Arusha. Aidha, Tanzania imewahi kuwa mwenyeji wa mikutano mingine mingi ya vyama vya kibunge ikiwemo ya IPU na CPA ambayo imeinufaisha nchi kwa kukuza diplomasia ya uchumi kupitia ugeni uliokuja lakini pia kufungua fursa mbalimbali za kitalii pamoja na kubadilishana uzoefu katika uendeshaji wa shughuli za kibunge.

### *Michezo ya Kitaifa na Kimataifa kwa Wabunge*

Michezo ni furaha, ni afya na pia ni muhimu katika kuwaunganisha watu popote duniani. Kwa waheshimiwa wabunge, michezo imekuwa sehemu ya maisha yao wakati wote wanapotekeleza majukumu ya kibunge. Miaka 60 ya muungano inapotimia hivi leo, bunge linajivunia kupiga hatua kubwa katika ushiriki wa wabunge katika michezo mbalimbali ndani na nje ya nchi, kama vile Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Michezo mingine inahusisha mabonanza mbalimbali yanayoandaliwa na Ofisi ya Bunge wakati wa mikutano ya bunge ambayo hufanyika Dodoma yakishirikisha wabunge na watumishi wa bunge.

Aidha, wabunge kutoka pande zote mbili za muungano wanashiriki katika michezo ya maadhimisho ya siku ya Mapinduzi ya Zanzibar Januari ya kila mwaka visiwani Zanzibar. Mabonanza hayo hushirikisha michezo ya soka, mpira wa pete, mpira wa kikapu, mpira wa nyavu, kurusha tufe, riadha, kuvuta kamba, gofu, drafti, pooltable, mpira wa meza, kurusha vishale, kufukuza kuku, kukimbia na magunia, na kutembea kwa mwendo wa haraka.

## *Kudumisha Utawala Bora*

Mojawapo ya misingi muhimu ya maendeleo ya taifa lolote ni kuzingatia utawala bora. Aidha, unapozungumzia utawala bora huwezi acha kugusa mambo muhimu kama vile uwazi na uwajibikaji ambapo katika maadhimisho ya miaka 60 ya muungano, bunge la muungano limekuwa kiungo muhimu katika kuhakikisha taifa linazingatia misingi ya utawala bora.

Kupitia majukumu yake ya kisheria, bunge limefanya kazi kwa karibu na serikali katika kuhakikisha uwajibikaji, uwazi, na uwakilishi wa wananchi katika mchakato wa kufanya maamuzi. Bunge hili limekuwa likishirikisha wananchi, kama wadau, katika vikao vya kamati wakati wa kupitia na kuchambua miswada mbalimbali ya sheria.

Vilevile ili kuhakikisha ushirikiano wa pande zote mbili za muungano unafuata misingi ya utawala bora, uteuzi na uchaguzi wa nafasi nafasi mbalimbali za uongozi bungeni unazingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni za Kudumu za Bunge zilizotungwa kwa mujibu ya Ibara ya 89 ya Katiba ya Tanzania. Mathalani, Kanuni ya 13(3) na 14 ya Kanuni za Kudumu za Bunge zinazoelekeza kuzingatia uwepo wa wajumbe kutoka pande zote mbili za muungano na uzingatiaji wa jinsia katika nafasi za wenyeviti wa bunge na uchaguzi wa wabunge wanaokwenda kwenye vyombo vingine vya uwakilishi.

## *Usimamizi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Serikali*

Kwa mujibu wa Ibara ya 62(2), na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bunge limepewa mamlaka ya kuisimamia na kuishauri serikali katika utekelezaji wa majukumu yake, pamoja na kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu unaokusudiwa kutekelezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ndani ya miaka hii 60 ya muungano, bunge limekuwa jukwaa la kujadili na kupitisha sera na mipango ya maendeleo ya kitaifa. Kupitia mjadala na uchambuzi wa kina, bunge limechangia kuimarisha na kuwezesha utekelezaji wa sera na mipango inayolenga kuinua ustawi na maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Usimamizi huu umekuwa ukifanywa kupitia shughuli za kamati za bunge ambazo taarifa ya utekelezaji wake huwasilishwa, kujadiliwa na kupitishwa na bunge.

Bunge limekuwa likitumia mamlaka yake ya kuisimamia na kuishauri serikali kwa kuunda kamati teule mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 139(1) na (2). Aidha, Kanuni ya 144(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imetoa nafasi kwa Mheshimiwa Spika kuunda kamati maalum ya kushughulikia jambo mahsusi. Mamlaka haya ya bunge yametoa nafasi pana ya bunge kuchunguza masuala yanayowatatiza wananchi na kuwa kikwazo cha maendeleo ya nchi; na kisha kutoa taarifa ya uchunguzi husika bungeni na halafu kutoa maazimio ambayo serikali inaelekezwa kuyatekeleza.

Miongongoni mwa kamati teule ambazo zimewahi kuundwa na bunge ni pamoja na kamati kuchunguza mchakato wa zabuni ya uzalishaji umeme wa dharura ulioipa ushindi kampuni ya Richmond Development Company LLC ya Houston, Texas, Marekani, mwaka 2008. Bunge limewahi pia kuunda kamati maalum mbalimbali ikiwemo; kamati ya kutathmini na kuangalia jinsi mpango wa kupambana na majangili ulivyopangwa na kutekelezwa na serikali kupitia operesheni tokomeza. Kamati hii iliundwa na spika kwa kutoa mamlaka kwa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kushughulikia suala hilo. Kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 117(18), toleo la 2013, iliunda kamati ndogo ya wabunge tisa wakisaidiwa na sekretariati ya Bunge ya watalaam wanne.

Kamati zingine maalum zilizoundwa na bunge ni pamoja na: kamati maluum iliyochunguza kashfa ya IPTL na kuhusishwa na uchotwaji wa shilingi bilioni 306 kutoka akaunti ya Tegeta Escrow; kamati maalum ya kufuatilia sekta ndogo ya gesi; kamati maalum ya uvuvi wa bahari kuu; kamati maalum ya madini ya tanzanite; na kamati maalum ya kufuatilia madini ya almasi.

Bunge la muungano limekuwa likipitisha mikataba mbalimbali yenye tija kwa taifa kama vile mkataba wa uwekezaji na uendelezaji wa bandari wa kampuni ya DP World; kuisimamia serikali katika miradi mikubwa ya kimkakati kama vile Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), mradi wa reli ya kisasa wa (SGR) na mingine mingi. Vilevile, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limewezesha maendeleo kwa kuanzisha Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDCF) ambao umekuwa chachu ya kuchochea maendeleo ya majimbo mengi hapa nchini.

## *Miundombinu ya Bunge*

Tunapoadhimisha miaka 60 ya muungano, tunashuhudia mafanikio makubwa katika uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu ikiwa ni pamoja na: ujenzi wa ukumbi mpya uliozinduliwa mwaka 2006 wenye uwezo wa kuchukua idadi ya wabunge zaidi ya 400 na wageni zaidi ya 300 kwa wakati mmoja; ujenzi wa kumbi za mikutano ya kamati, ofisi za watumishi, uwekaji wa kambarau katika jengo kuu la utawala na jengo dogo la utawala; usimikaji wa miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo imewezesha matumizi ya vifaa vya kisasa kama vile simu, kompyuta mpakato, skana, vishikwambi, na runinga.

Vilevile, Ofisi ya Bunge imewezesha matumizi ya bunge mtandao ambao umepunguza matumizi makubwa ya karatasi. Aidha, Ofisi ya Bunge imeongeza umiliki wa eneo la viwanja vya bunge kutoka la awali na kuchukua maeneo yote ya karibu yanayolizunguka. Hapo awali, bunge lilikuwa na eneo la ukubwa wa meta za mraba 42,000, lakini sasa eneo hilo limeongezwa na kufikia meta za mraba 154,000, sawa na ongezeko la asilimia 72.7.

*Wageni Wanaotembelea Bunge*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekuwa ni moja ya sehemu inayoitambulisha nchi kimataifa kutokana na wageni wengi wakiwemo wakuu wa nchi mbalimbali kuvutiwa kutembelea mhimili huu wa nchi. Ujio wa wageni hawa umechagizwa na amani na utulivu uliopo nchini pamoja na umaarufu ambao nchi yetu imejijengea katika taswira ya kimataifa katika suala zima la diplomasia na ushirikiano wa kimataifa. Watu wengi wamekuwa wakitembelea kwa madhumuni mbalimbali ikiwemo kujifunza, kupata uzoefu na kukuza mahusiano bora ya kidiplomasia.

Miongoni mwa wageni waliolitembelea Bunge la Tanzania na kupata nafasi ya kulihutubia ni pamoja na wakuu au waliokuwa wakuu wa nchi wafuatao: Mhe. Daniel Arap Moi aliyekuwa Rais wa Kenya, alilihutubia Bunge jijini Dodoma mwaka 2005; Mhe. Mary McAleese aliyekuwa Rais wa Ireland ambaye alilihutubia Bunge tarehe 22 Juni 2006; Mhe. Ahmed Abdallah Mohamed aliyekuwa Rais wa Komoro aliyelihutubia Bunge tarehe 25 Agosti 2008; na Mhe. Felipe Nyusi, Rais wa Msumbiji ambaye alilihutubia Bunge tarehe 20 Mei, 2015.

*Mustakabali wa Bunge kwa Siku Zijazo*

Safari ya mafanikio na maendeleo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano hajakomea hapo, bali sasa kadri miaka inavyosonga mbele, ndivyo maendeleo na mafanikio yatazidi kukua na kuongezeka, kama ambavyo sasa Bunge limeongeza umiliki wa eneo lake jijini Dodoma na pia linapanga kujenga Jengo la Makumbusho ya Bunge katika viwanja vya Bunge.

Bunge la Tanzania litaendelea kuongeza mafanikio katika nyanja za uchumi, siasa, kijamii, na kiutamaduni, na daima litakuwa nguzo imara ya kudumisha muungano na kuwaletea mafanikio Watanzania wa pande zote mbili za Muungano.

Ili kuzungumzia mafanikio ya Bunge kwa miaka 60 ya muungano, pengine ingelifaa kuandika kitabu cha kurasa nyingi ambazo zingegusa kila hatua ya maendeleo tangu bunge la muungano liundwe mwaka 1964, na kuorodhesha majina ya wote waliotekeleza mambo mbalimbali na kulifanya liwe la ufanisi kama lilivyo sasa. Hata hivyo, kwa sasa haya mafanikio yanalolifanya Bunge la Jamhuri ya Muungano kuwa miongoni mwa machache ya kuigwa, kama ambavyo imeshuhudiwa wageni mbalimbali, hasa watalaam na wabunge kutoka mabunge mengine kuomba kutembelea bunge kwa ajili ya kujifunza kutokana na mafanikio hayo yaliyofikiwa kwa miaka 60 ya muungano.

393

**Idadi ya wabunge, Bunge la Tanganyika na Zanzibar**

301%

**Ongezeko kwa asilimia ndani ya Bunge la Tanganyika na Zanzibar**

78

**idadi ya wabunge wa Zanzibar ndani ya bunge la muungano kwa sasa**

20%

**Asilimia ya wabunge wa Zanzibar ndani ya bunge la muungano kwa sasa**

**kila idadi ya jumla inapoongezeka na idadi ya wabunge wa Zanzibar nayo pia inaongezeka.**

*Upekee wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa wa kipekee duniani kwani ulifikiwa kwa makubaliano ya hiari baina ya wananchi wa nchi mbili huru na sasa umedumu kwa zaidi ya nusu karne. Miungano mingine duniani kama ya Marekani, Uingereza au Imarata (UAE), haikufikiwa kwa njia hii bali mazingira tofauti.*



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson

# NIDA Yafungua Ofisi 153 *Tanzania Bara, Zanzibar*

Na Mwandishi Wetu

Wakati Tanzania inaadhimisha miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio ya maadhimisho hayo baada ya kufanikiwa kufungua ofisi 153 katika wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar, ikiwemo kuziunganisha ofisi za wilaya 152 na kituo cha uchakataji taarifa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

NIDA imesogeza pia huduma ya usajili na utambuzi kwa kufungua ofisi katika maeneo yenye wakazi wengi ya Morogoro vijijini, Itigi na Chalinze, ili kuwaondolea wananchi hao usumbufu wa kufuata huduma wilayani na bado inaendelea kusogeza huduma hizo katika maeneo mengine yenye idadi kubwa ya watu.

Msemaji wa NIDA, Geofrey Tengeneza, anaeleza kuwa lengo la kuunganisha ofisi za wilaya 152 na kituo cha uchakataji taarifa ni kuwezesha mawasiliano kati ya ofisi za usajili, na kuhakikisha maombi ya watu wote waliosajiliwa yanasafirishwa kutoka ofisi za usajili za wilaya kwenda Kituo cha Kuchakata Taarifa kwa ajili ya uchakataji na uzalishaji vitambulisho kwa wakati.

Tengeneza amesema NIDA imefanikiwa kuunganisha mfumo wake na taasisi kadhaa za umma na binafsi katika mfumo wa usajili na utambuzi wa watu, ambapo jumla ya taasisi 96 zikiwemo tatu za Zanzibar zimeunganishwa katika mfumo kwa lengo la kurahisisha utoaji huduma na utambuzi wa wananchi wanaopata huduma katika taasisi hizo na kwamba hivi sasa watu wote wenye utambulisho wa taifa (NIN) wanaweza kupata huduma zote wanazostahili nchini.

Katika kipindi hiki, NIDA imefanikiwa kujenga kituo kikubwa cha kuhifadhi taarifa za watu (Data Centre) ambacho kimekuwa chachu ya ongezeko la usajili na utambuzi wa watu. Pia imejenga kituo cha uokozi (Data Recovery Centre), kikifanya kazi sambamba na kituo cha uchakataji taarifa.

Katika kuboresha huduma za usajili na utambuzi, NIDA imeanzisha huduma ya usajili mtandaoni (online registration) kupitia online.nida.go.tz. Mfumo huo ulianza kutumika mwaka 2022/2023 na umeonesha ufanisi huku ukisaidia kupunguza uhitaji wa wananchi kwenda kusajili katika ofisi za NIDA za wilaya.
Vilevile, Mamlaka hiyo imefanikiwa kuwasajili Watanzania wanaoishi nje ya nchi ambao bado hawajakana uraia wao wanaojulikana kama. Usajili huu wa majaribio ulifanyika katika nchi za Marekani, Uingereza na Uholanzi. Hii ni hatua kubwa ikiwa ni kuunga mkono maombi ya Watanzania waishio nje ya nchi kusajiliwa ili washiriki vema katika shughuli za kiuchumi nchini.



Eneo lingine la mafanikio ambalo NIDA inajivunia ni ujenzi wa mifumo ya usajili na utambuzi. Katika kufanikisha mkakati wa mamlaka wa kujitegemea kimfumo na kuimarisha mfumo wa vitambulisho vya taifa, mamlaka kwa kutumia wataalamu wa ndani imefanikiwa kujenga mifumo 24 kati ya mifumo 42 inayokusudiwa kujengwa. Mifumo hiyo imesaidia kuondokana na utegemezi wa mkandarasi na hivyo kuokoa fedha za serikali.

Mifumo hiyo pia imewezesha mamlaka kuondokana na ukomo wa leseni ya matumizi katika mifumo ya vitambulisho vya taifa, kumiliki nakala halisi ya programu za mfumo wa vitambulisho vya taifa na kufanya maboresho ya mfumo pindi yanapohitajika.

Mafanikio mengine ni kuwezesha matumizi ya mfumo wa usajili na utambuzi kwa kutumia taarifa za kanzidata katika masuala ya ulinzi na usalama nchini; kusaidia kupambana na ufadhili wa ugaidi na utakatishaji wa fedha kwa kuhakikisha laini za simu zinasajiliwa kwa kutumia utambulisho wa taifa; akaunti za benki zinafunguliwa kwa kutumia namba ya utambulisho wa taifa; kuwezesha kupambana na makosa ya kimtandao pamoja; na kusaidia vyombo vya ulinzi na usalama katika kutekeleza majukumu yao.

Katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, mamlaka imesajili na kutambua jumla ya watu 24,495,804 hadi Februari, 2024, ambapo kati ya hao watu 20,832,225 wamepatiwa namba za utambulisho (National Identification Number - NIN), kiasi ambacho ni sawa na asilimia 84.8 ya watu wote waliosajiliwa.

Aidha, mamlaka imefanikiwa kuzalisha vitambulisho 20,286,420 kati ya namba za utambulisho 20,832,225, sawa na asilimia 97.4.

NIDA ambayo ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ndiyo yenye jukumu kuu la kusimamia suala la usajili na utambuzi wa watu pamoja na utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi, wageni wakaazi pamoja na wakimbizi halali wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

# 24,495,804

**Watu waliyosajiliwa na kutambuliwa na kipindi cha miaka 60 (Hadi Februari 2024)**

# 20,832,225

**Idadi ya watu waliyopatiwa namba za utambulisho (National Identification Number - NIN) ni sawa na 84.8%**

# 20,286,420

**Idadi ya vitambulisho vilivyozalishwa ndani ya kipindi cha miaka 60 (Hii ni sawa na 97.4%)**



*NIDA imefungua ofisi 153 katika wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar*

*Ofisi za wilaya 152 zimeunganishwa na kituo cha uchakataji taarifa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi*





# TANESCO, ZECO *Kuongeza Wigo wa Ushirikiano*

**TANESCO itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) katika kutekeleza miradi ya kimkakati**

Na Mwandishi Wetu, TANESCO

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga, amesema kuwa katika kipindi kifupi kijacho mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) utaongeza kiwango cha nishati ya umeme kupitia gridi ya taifa na hatimaye kuongeza upatikanaji umeme Tanzania Bara na Zanzibar.

Mhandishi Nyamo-Hanga amesema kuwa wakati huu ambapo Zanzibar imetimiza miaka 60 ya mapinduzi matukufu na ndio mwaka ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nayo inatimiza miaka 60, TANESCO itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) katika kutekeleza miradi ya kimkakati na kuhakikisha panakuwepo na usambazaji bora wa nishati ya umeme kwa wananchi wa Zanzibar ili kuchochea shughuli za kiuchumi.

Amesema tangu mwaka 1980 wakati njia ya kwanza ya usafirishaji umeme kutoka kituo cha Ubungo, Dar es Salaam, ilipojengwa kwenda Unguja, TANESCO na ZECO zimekuwa zikishirikiana kuhakikisha Zanzibar inasambaziwa nishati ya umeme ya kutosha kwa kuzingatia dira ya serikali, ambayo kwa sasa inaangazia mwaka 2050.

Katika kuendeleza ushirikiano huo, Mhandisi Nyamo-Hanga amesema tarehe 12 Novemba, 2023, Wizara ya Nishati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar zilisaini Hati ya Makubaliano kwa lengo la kuongeza ushirikiano katika masuala ya nishati ikiwemo uzalishaji umeme, shughuli za uendeshaji, ukarabati, usaidizi wa kiufundi, mafunzo na kujengeana uwezo.

Aidha, tarehe 15 Februari, 2022, Shirila la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilisaini Hati ya Makubaliano na Shirika la Maendeleo ya Petroli Zanzibar (ZPDC). Makubaliano hayo yalikuwa katika maeneo ya ushirikiano wa kitaalam, kujenga uwezo wa wataalam wa ZPDC na kubadilishana uzoefu.

Mhandisi Nyamo-Hanga alisema zaidi kuwa tangu makubaliano hayo yasainiwe, mambo mengi yametekelezwa ikiwa ni pamoja na kuunda kamati ya pamoja ya usimamizi na utekelezaji wa makubaliano yenye wajumbe 11, kati yao watano wanatoka TPDC na sita wanatoka ZPDC.

Hivi sasa wataalam wa ZPDC wamekuwa wakija Tanzania Bara kujifunza masuala mbalimbali yakiwemo ya uchimbaji na ukusanyaji wa taarifa za mitetemo; mafunzo ya namna ya kuchakata na kutafsiri taarifa za mitetemo; mafunzo ya uhifadhi wa taarifa za utafiti; kuandaa miongozo ya utunzaji wa taarifa kwa ajili ya wataalam wa ZPDC; mafunzo ya manunuzi ya vifaa mbalimbali; na mifumo katika eneo la utafiti na uchimbaji wa gesi asilia na mafuta.

TPDC pia imeshirikiana na ZPDC kuandaa na kushiriki katika kongamano la mafuta na gesi lililofanyika Zanzibar na pia menejimenti na bodi za TPDC na ZPDC zinaendelea kushirikiana kwa pamoja kwenye masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi.
Mhandisi Nyamo-Hanga anatoa historia fupi ya umeme Zanzibar, kwa kusema kuwa mwaka 1908 kisiwa cha Unguja kilikuwa kikipata umeme kupitia mitambo ya kuzalisha nishati ya umeme kwa nguvu za makaa ya mawe, ikiwa chini ya Bodi ya Umeme Zanzibar.
Ameeleza kuwa mwaka 1954 mitambo hiyo iliondolewa na mitambo ya kuzalisha nishati ya umeme kwa mafuta ya dizeli ikaanza kutumika.
"Mwaka 1964 Shirika la Nishati na Mafuta la Zanzibar (ZSFPC) lilianzishwa na ilipofika mwaka 1980 kisiwa cha Unguja kikaungwa na njia ya umeme kutoka Tanzania Bara ya msongo wa kilovoti 132 na uwezo wa megawati 45 kupitia njia ya chini ya bahari, kutoka Rasi Kilomoni Salaam hadi Rasi Fumba yenye urefu wa kilomita 37," anabainisha Mhandisi Nyamo-Hanga.
"Mwaka 2013 njia ya pili ya umeme inayopita chini ya bahari yenye msongo wa kilovoti 132 na uwezo wa megawati 100 ilijengwa," anaeleza zaidi.

Akielezea historia ya upatikanaji umeme kisiwani Pemba, Mhandisi Nyamo-Hanga alieleza kuwa mwaka 1958, mtambo wa kwanza wa kuzalisha umeme ulisimikwa katika eneo la Tibirinzi kisiwani Pemba.

Aidha, anasema mwaka 1985 kilianzishwa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito cha Wesha kilichokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 4.5. Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO anabainisha kuwa mwaka 2010 kisiwa cha Pemba kiliunganishwa na gridi ya taifa kutoka Tanzania Bara kupitia njia ya msongo wa kilovoti 33 na uwezo wa megawati 16 yenye urefu wa kilomita 75 chini ya bahari kutokea Majani Mapana mkoani Tanga. Hatua hii ilisababisha kuzimwa kwa kituo cha kuzalisha umeme cha Wesha.

Kutokana na ongezeko la shughuli za uwekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, Mhandisi Nyamo-Hanga ameeleza kuwa mahitaji ya nishati ya umeme yameongezeka Zanzibar hivyo kuchagiza ongezeko la mahitaji ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali.

Aidha, Mhandisi Nyamo-Hanga amesema serikali inatarajia kujenga mradi wa njia ya msongo wa kilovoti 220 itakayopita chini ya bahari itakayokuwa na uwezo wa kusafirisha megawati 240 kutoka Tanzania Bara hadi Zanzibar ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme katika kisiwa cha Unguja. Mradi huu uko katika hatua za awali za upembuzi yakinifu.

Alieleza zaidi kuwa mradi mwingine ni wa njia ya msongo wa kilovoti 132 itakayopita chini ya bahari yenye uwezo wa kusafirisha megawati 150 kutoka Tanga hadi kisiwa cha Pemba.

Mhandisi Nyamo-Hanga alimalizia kwa kusema kuwa njia hizo zitapita katika eneo ambalo njia za sasa za kusafirisha umeme zimepitia chini ya bahari.

** Mwaka 2010 kisiwa cha Pemba kiliunganishwa na gridi ya taifa kutoka Tanzania Bara kupitia njia ya msongo wa kilovoti 33 na uwezo wa megawati 16 yenye urefu wa kilomita 75 chini ya bahari kutokea Majani Mapana mkoani Tanga. Hatua hii ilisababisha kuzimwa kwa kituo cha kuzalisha umeme cha Wesha.*



# *Usahihi wa Utabiri Hali ya Hewa Nchini* Wafikia Asilimia 98

Katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kuimarisha na kuboresha utoaji na usambazaji wa huduma za hali ya hewa nchini na hivyo kuongeza kiwango cha usahihi wa utabiri wake hadi wastani wa asilimia 98 kufikia mwaka 2023.
Kiwango hicho kimepanda kutoka viwango vya usahihi wa utabiri kutoka asilimia 87.5 mwaka 2014. Wastani wa usahihi wa aslimia 98 ni juu ya kiwango cha juu cha usahihi kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa la Dunia (WMO) ambacho ni asilimia 70.

Mafanikio hayo ni kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika kwa kununua na kusimika mitambo ya kisasa ya uangazi na kuchakata taarifa za hali ya hewa.
Mwaka 1964 kulikuwa na kituo kikuu kimoja Dar es Salaam kilichokuwa kinafanya kazi kwa saa 24 lakini hivi sasa Tanzania inapotimiza miaka 60 ya muungano kuna vituo 27 vya kupimia hali ya hewa; vituo 476 vya kupimia mvua; vituo 49 vinavyojiendesha vyenyewe; vituo 13 vya kilimo na vituo aba vya bandari kwenye bahari na maziwa makuu ikiwemo bandari ya mkoani Pemba na Malindi, Unguja.

> Mwaka 1964 kulikuwa na kituo kikuu kimoja Dar es Salaam kilichokuwa kinafanya kazi kwa saa 24 lakini hivi sasa Tanzania inapotimiza miaka 60 ya muungano kuna vituo 27 vya kupimia hali ya hewa; vituo 476 vya kupimia mvua; vituo 49 vinavyojiendesha vyenyewe; vituo 13 vya kilimo na vituo aba vya bandari kwenye bahari na maziwa makuu ikiwemo bandari ya mkoani Pemba na Malindi, Unguja.

Zaidi ya asilimia 80 ya vifaa vyenye teknolojia ya kisasa (kidijiti) vimefungwa katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na matakwa ya kimataifa (MINAMATA) ya kuondosha matumizi ya zebaki.
Mwaka 2010 serikali ilianza mchakato wa kufunga mitambo saba ya kisasa ya rada za hali ya hewa, ambapo mpaka hivi sasa mamlaka imefanikiwa kufunga rada tano katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Kigoma na Mbeya.
Utengenezaji wa rada zingine mbili zitakazofungwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma unaendelea kiwandani nchini Marekani na zinatarajiwa kukamilika na kufungwa mwaka huu. Hatua hii inaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki kuwa na mtandao mkubwa wa rada.

Aidha, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu, umefanyika ununuzi, ufungaji na mafunzo maalum ya matumizi ya kompyuta yenye uwezo mkubwa wa kuchakata taarifa za hali ya hewa. Kompyuta hii kubwa ambayo ni ya kisasa na ni ya mfano barani Afrika, inaiwezesha TMA kuboresha shughuli za hali ya hewa, hususani ongezeko la usahihi na uwezeshaji wa utabiri wa maeneo madogo madogo, ambapo huduma hiyo imeshaanza katika ngazi ya wilaya kwenye utabiri wa msimu.

Sambamba na mafanikio hayo, serikali imeendelea kuwekeza katika usalama wa anga la nchi yetu kwenye upande wa huduma za hali ya hewa kwa kufanikisha ununuzi na kufungwa kwa vifaa vya kisasa vya hali ya hewa (Avimet) vinavyosaidia kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa kwa ndege zinazoruka na kutua.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ndani ya miaka 60 ya muungano ni kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019, na kuanza kutumika tarehe 14 Juni, 2019, kupitia Tangazo la Serikali Na. 459 la mwaka 2019 ambako kumeimarisha sekta hali ya hewa nchini.
Kupitia sheria hiyo TMA imeongezewa majukumu ya kudhibiti na kuratibu shughuli zote za hali ya hewa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa lengo la kuhakikisha miongozo yote ya kitaifa na kimataifa inasimamiwa.

Pia serikali imefanikisha uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma, ambacho ni cha pili kuanzishwa katika ukanda wa Afrika Mashariki kati ya vitatu vilivyopo katika ukanda huo.
Chuo hiki kinaendelea na maandalizi ya mafunzo mahsusi ya rada na matumizi yake katika utabiri kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Mafunzo haya ni fursa kutoka Shirika la Hali ya Hewa la Dunia (WMO) kwa Tanzania kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali wa kuimarisha miundombinu ya hali ya hewa, hususani rada za hali ya hewa.

Kwa upande wa watumishi, mwaka 1964, taasisi ya hali ya hewa kwa nchi zote za Afrika Mashariki zilikuwa na wafanyakazi 330 ambapo kati yao wanasayansi na wataalamu bobezi wa hali ya hewa walikuwa 14 tu na hapakuwa na mtaalamu mbobezi mzalendo wa hali ya hewa, lakini hadi kufika sasa TMA ina jumla ya watumishi 525, kati yao wataalamu wabobezi wa hali ya hewa ni 402.

Sambamba na hayo, kwa mara ya kwanza ujenzi wa jengo la kanda ya Mashariki na kituo cha kufuatilia matukio ya Tsunami umeanza kutekelezwa ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 38.

Mamlaka ipo katika maadalizi ya ujenzi wa jengo la hali ya hewa pamoja na kituo cha kutoa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa (Climate Analysis and Early Warning Centre) katika jiji la Dodoma na litakapokamilika litasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa pamoja na mfumo wa kutoa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa nchini.

TMA imeendelea kuboresha huduma na hivyo kufanikiwa kupata cheti cha ubora katika utoaji wa huduma za hali ya hewa katika sekta ya usafiri wa anga (ISO 9001: 2015) mnamo tarehe 30 Januari, 2018, baada ya ukaguzi wa kimataifa uliofanyika mwezi Desemba 2017; na hivyo kuthibitisha kuwa huduma za hali hewa zinatolewa na TMA ni sahihi, zenye ubora mkubwa na zinazokidhi viwango vya kimataifa.

Tanzania kupitia TMA ni nchi ya tatu barani Afrika kwa taasisi za hali ya hewa kupata cheti hicho ikitanguliwa na Nigeria na Afrika Kusini. TMA imeendelea kukaguliwa kila mwaka na katika ukaguzi uliofanyika mwezi Januari 2024, TMA imeendelea kushikilia cheti hicho cha ubora

TMA imeendelea kuboresha huduma na hivyo kufanikiwa kupata cheti cha ubora katika utoaji wa huduma za hali ya hewa katika sekta ya usafiri wa anga (ISO 9001: 2015) mnamo tarehe 30 Januari, 2018, baada ya ukaguzi wa kimataifa uliofanyika mwezi Desemba 2017



Zaidi ya asilimia 80 ya vifaa vyenye teknolojia ya kisasa (kidijiti) vimefungwa katika maeneo mbalimbali nchini kulingana na matakwa ya kimataifa (MINAMATA) ya kuondosha matumizi ya zebaki.

Mwaka 1964, takwimu zote za hali ya hewa zilikuwa zinahifadhiwa Nairobi nchini Kenya na mwaka 1972, kiasi kikubwa cha taarifa hizo kilifanikiwa kurejeshwa nchini na kuhifadhiwa katika mifumo ya makbrasha, magnetic tapes na punch-crads; na kuanzia mwaka 1990, TMA ilianza kuhifadhi na kuchambua takwimu za hali ya hewa kwa kutumia teknolojia za kisasa kama vile CLICOM na baadaye CLIDATA na ELO. Mabadiliko hayo yamefanikisha uokoaji na upataikanji wa takwimu nyingi za hali ya hewa zilizopo kuanzia mwaka 1892 hadi sasa.

TMA imeendelea kupeperusha bendera ya Tanzania kimataifa. Hivi karibuni, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Ladislaus Chang'a, alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) katika uchaguzi wa viongozi wapya uliofanyika mwezi Julai 2023, jijini Nairobi, Kenya. Kuchaguliwa kwake kunaonesha mahusiano mazuri ya serikali katika nyanja za kimataifa.

Kwa ufupi mafanikio makubwa yamepatikana katika kipindi hiki cha miaka 60 ya muungano katika sekta ya hali ya hewa na hivyo, kuifanya TMA kuwa taasisi ya mfano barani Afrika na nchi nyingi kuja kujifunza hapa nchini. Wataalamu wa wa hali ya hewa yan chi yetu wamesaidia baadhi ya nchi barani Afrika na nje ya bara la Afrika kuboresha huduma zao. Nchi hizo ni Namibia, Libya, Nigeria, Saudi Arabia na Maldives.



# *Mafanikio ya Tasnia ya Takwimu katika* Miaka 60 ya Muungano

**Katika orodha ya masuala ya muungano, takwimu ni suala la 20. Makala hii inaangalia maendeleo ya tasnia ya takwimu, mchango wake katika maendeleo na namna takwimu zilivyosaidia kuimarisha muungano wa Tanzania.**

Na Said Ameir, NBS

Tunapozungumzia mafanikio ya miaka 60 ya muungano hatuwezi kuiacha tasnia ya takwimu ambayo ndiyo moyo na macho ya serikali katika kupanga, kufanya maamuzi, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Karibu duniani kote takwimu rasmi huzalishwa, huratibiwa na kusambazwa na ofisi za takwimu za nchi husika ambazo zimepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya hivyo.

Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar (OCGS), ndizo zenye mamlaka ya kuzalisha, kuratibu uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi ndani ya Mfumo wa Taifa wa Takwimu kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura 351 na Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2007 kwa Tanzania Zanzibar.

Takwimu zinazotolewa au zinazoratibiwa na taasisi hizi ndizo zinazotumiwa na serikali na wadau kama takwimu rasmi katika kuandaa na kuhuisha sera, kupanga, kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo.

Wadau wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi wanaotumia takwimu hizo ni pamoja na sekta binafsi, jumuiya za wafanyabiashara, Umoja wa Mataifa, jumuiya za kimataifa na kikanda za nchi za Afrika, asasi za kiraia na wananchi kwa ujumla.

Kabla ya muungano, masuala ya takwimu kwa upande wa Tanganyika na Zanzibar yaliendeshwa kwa utaratibu tofauti kulingana na mifumo iliyorithiwa kutoka kwa tawala za kikoloni na mabadiliko yaliyofanywa baada ya uhuru na mapinduzi matukufu ya Zanzibar.

Masuala ya takwimu yaliongezwa katika orodha ya mambo ya muungano kwenye mabadiliko ya katiba ya mwaka 1977, na huo ukawa mwanzo wa ushirikiano wa karibu kati ya NBS na OCGS, ushirikiano ambao umekuwa ukiimarika siku hadi siku na kufanya taasisi hizi mbili kuwa kati ya taasisi za mfano wa kuigwa.





# 9,321,296

Makadirio ya idadi ya watu mwaka 1963 (kabla ya muungano)

# 9,624,401

Makadirio ya idadi ya watu mwaka 1964 (kipindi cha muungano)

# 3,601,105

Idadi ya watu waliokuwepo wakati wa muungano mwaka 1964, ikiwa ni miaka 60 hadi sasa (imepungua kutoka 9,624,401)

# 62,046,535

Makadirio ya idadi ya watu waliozaliwa baada ya muungano (wanaume ni 30,378,046 na wanawake ni 31,668,489)



Hata hivyo, kumbukumbu zinaonesha kuwa sensa ya mwaka 1967 ambayo ni ya kwanza baada ya muungano ilifanikishwa kupitia kazi nzuri iliyofanywa na wataalamu wa pande zote mbili za muungano, na pia kwa mchango mkubwa na ushirikiano wa wanachama wa vyama vya siasa vya TANU (Tanganyika African National Union) cha Tanzania Bara na ASP (Afro-Shirazi Party) cha Zanzibar, vyama viwili vilivyokuja kukiunda Chama Cha Mapinduzi (CCM) baadaye mwaka 1977.
Kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu sura 351, jukumu la kwanza la NBS ni kuandaa sensa ya watu na makazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, kila baada ya miaka kumi ambapo tangu sensa ya kwanza mwaka 1967 hadi sensa ya sita ya mwaka ya 2022, utekelezaji wake umekuwa wa mafanikio kwa ushirikiano kati ya taasisi hizo mbili za takwimu nchini. Sensa zingine za watu na makazi zilifanyika nchini katika miaka ya 1978, 1988, 2002 na 2012.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, wakizindua nembo na tarehe ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar

Kwa msingi huo, mafanikio makubwa ya NBS katika kipindi cha miaka 60 ya muungano yapo kisheria na ni kuwezesha upatikanaji wa takwimu rasmi kwa ajili ya kutunga sera, kupanga mipango ya maendeleo, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake ili kuboresha maisha ya Watanzania.

Takwimu hizo zimeiwezesha serikali na wadau kubuni na kutekeleza mipango ya kimkakati ambayo imechangia kuongeza fursa za kiuchumi nchini kama vile uwekezaji ambao nao umechangia kuendelea kuimarika kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Pato la Jumla la Taifa (GDP) kwa ujumla, kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za kijamii za kisekta kama vile kuongezeka kwa miundombinu na huduma bora za afya, elimu, maji, barabara, umeme na nyingine kwa lengo la kupambana na maadui watatu wa maendeleo ambao ni ujinga, umaskini na maradhi.

Mipango ya maendeleo ambayo imekuwa ikiandaliwa kuanzia mwaka 1964 hadi 2024 iwe ya muda mfupi, muda wa kati au muda mrefu zikiwemo Dira za Taifa za Maendeleo imekuwa ikizingatia takwimu zinazozalishwa na NBS na OCGS kwa ajili ya kuhakikisha haki na usawa katika ugawaji wa keki ya taifa ili kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

Miongoni mwa mipango hiyo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA I na MKUKUTA II), Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya miaka mitano na mikakati ya kisekta katika sekta mbalimbali kama elimu, afya, maji na nishati. Aidha, takwimu rasmi zimetumika kama msingi wa kufanya maamuzi katika miradi mikubwa ya kimkakati na ya muda mrefu ya taifa kama vile reli ya kisasa (SGR) na mabwawa ya kufua umeme kama la Julius Nyerere.

Takwimu rasmi ndizo zinazoweza kuonesha mwenendo wa mabadiliko katika viashiria muhimu vya maendeleo ya watu kama vile idadi ya watu kwa umri na jinsi, ukuaji wa uchumi na hali ya umaskini katika kipindi kimoja na kingine na kwa mapana yake kwenye nyanja za kijamii, kiuchumi na mazingira.

Vilevile, takwimu hizo zinatumika katika kufuatilia na kutathmini programu za maendeleo za kikanda na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Afrika Mashariki ya mwaka 2050, Dira ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063 na Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya Dunia ya mwaka 2030.

** Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar (OCGS), ndizo zenye mamlaka ya kuzalisha, kuratibu uzalishaji na usambazaji wa takwimu rasmi ndani ya Mfumo wa Taifa wa Takwimu kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura 351 na Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2007 kwa Tanzania Zanzibar.*

Ni dhahiri kuwa moja ya misingi ya mafanikio ya tasnia ya takwimu nchini ni utashi wa kisiasa wa viongozi wa Tanzania katika awamu zote sita kuanzia uongozi wa awamu ya kwanza ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume.
Aidha, katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, tasnia ya takwimu nchini imepitia mabadiliko makubwa kufuatia hatua za serikali za kuboresha na kuimarisha mfumo wa taifa wa takwimu nchini pamoja na kasi ya ongezeko la matumizi ya teknolojia duniani katika shughuli za ukusanyaji, uchakataji na usambazaji wa takwimu.

NBS kwa kushirikiana na OCGS imefanikiwa kupanua wigo wa uzalishaji wa takwimu rasmi zinazokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa katika maeneo yote matatu iliyopewa mamlaka kisheria; ambayo ni takwimu za kiuchumi, kijamii na mazingira.
Katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha kuwekeza rasilimali nyingi kwenye miundombinu ya kitakwimu, kuwajengea uwezo watumishi katika tasnia ya takwimu na kufanya marekebisho ya sheria za takwimu na kuzipatia NBS na OCGS mamlaka zaidi za kiutendaji.

Mafanikio mengine yaliyofikiwa ni kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya teknolojia katika ufanyaji wa sensa na tafiti mbalimbali nchini; uandaaji wa takwimu za kiutawala; na usambazaji wa takwimu rasmi kwa wadau. Kwa mfano, sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022 ilikuwa ni ya kidijitali ambapo teknologia ilitumika katika hatua zote za utekelezaji wake. Hii ni pamoja na wakati wa utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu na maswali yote kuingizwa katika vishikwambi na kufanikisha upatikanaji wa matokeo ya mwanzo ndani ya siku 45 tu baada ya zoezi la kuhesabu watu. Haya ni mafanikio makubwa ambayo hayajawahi kutokea katika historia ya sensa nchini na barani Afrika kwa ujumla.

Vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Awamu ya Kwanza ya Mpango Kabambe wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania (Tanzania Statistical Masterplan – TSMP I) ambao ulitekelezwa kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 hadi 2017/18.

Miongoni mwa mafanikio ya TSMP I ni pamoja na kupatikana kwa Sheria ya Takwimu Sura 351; kuboresha mazingira ya kazi ikiwemo ujenzi wa majengo ya kisasa ya takwimu yaliyojengwa Dodoma na Unguja; kuboreshwa kwa upatikanaji wa takwimu rasmi ambapo tathmini ya Benki ya Dunia mwaka 2016/17 ilionesha kuwa Tanzania ilikuwa nchi ya pili barani Afrika kwa uzalishaji wa takwimu bora baada ya Afrika ya Kusini.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Waziri Kindamba, ufunguo wa gari la kubebea wagonjwa wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania wa Mwaka 2022 jijini Dar es Salaam.

Katika kuthibitisha dhamira yake ya kuendelea kuimarisha tasnia ya takwimu nchini, serikali ya awamu ya sita chini uongozi wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeridhia kuendeleza mafanikio ya mpango wa kwanza na kutumia changamoto zilizobainishwa kama fursa ya kuimarisha tasnia ya takwimu nchini kwa kuidhinisha utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango Kabambe wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania (TSMP II). Utekelezaji wa TSMP II utafanyika katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2026/2027(Tanzania Statistical Masterplan-TSMP II 2022/2023-2026/2027).

Malengo ya TSMP II ni kuimarisha zaidi Mfumo wa Taifa wa Takwimu katika maeneo ya ulinganishi wa takwimu katika wizara, idara na taasisi za serikali; kuongeza mifumo ya ukusanyaji wa takwimu katika wizara, idara na taasisi za serikali hususan taarifa za kiutawala; na uimarishaji wa miundombinu ya kitakwimu kwa maana ya majengo na mifumo ya tekinolojia katika utekelezaji wa shughuli za kitakwimu.




Jengo la Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) lililopo Barabara ya Lusinde jijini Dodoma,

Katika utekelezaji wa TSMP II, Serikali imepanga kujenga majengo mapya matatu katika mikoa ya Lindi, Simiyu na kisiwani Pemba ili kuendelea kupeleka huduma na shughuli za kitakwimu karibu na wananchi, kuongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji na usambazaji wa takwimu nchini.

Aidha, katika kuimairisha ushirikiano kati ya NBS na OCGS, Mwenyekiti wa Bodi ya Takwimu Zanzibar na Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar ni wajumbe wa Bodi ya Usimamizi ya NBS kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Sura 351. Maboresho haya yamekusudia kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano wa moja kwa moja katika uendeshaji wa shughuli za kitakwimu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vilevile, katika kipindi chote baada ya muungano, kumekuwepo na vikao vya pamoja kati ya menejimenti za ofisi za takwimu kwa pande zote mbili za muungano ili kuimarisha ushirikiano katika kuzalisha na kusambaza takwimu rasmi nchini zinazoakisi hali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Viongozi wengi wa kitaifa wamekuwa wakisistiza kwamba ushirikiano kati ya NBS na OCGS ni miongoni mwa mifano ya taasisi zinazoimarisha muungano nchini; hivyo, taasisi nyingine zinaweza kujifunza na kutekeleza kwa ajili ya maendeleo jumuishi ya nchi yetu.
Ni vyema pia katika maadhimisho ya miaka 60 ya muungano, takwimu za idadi ya watu na tafsiri yake, hususan historia yake na hali ilivyo mwaka 2024, zikafahamika.
Kabla ya muungano mwaka 1964, idadi ya watu kwa mwaka 1963 ilikadiriwa kufikia 9,321,296 ambapo kati ya watu hao, wanaume walikuwa 4,252,227 na wanawake 5,069,069, sawa na asilimia 45.6 kwa 54.4, mtawalia.

Wakati wa muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, idadi ya watu ilikadiriwa kufikia 9,624,401 ambapo kati yao wanaume walikuwa 4,390,499 na wanawake 5,233,902, sawa na asilimia 45.6 kwa 54.4 mtawalia.
Idadi ya watu waliokuwepo wakati wa muungano mwaka 1964, ikiwa ni miaka 60 hadi sasa, imepungua kutoka 9,624,401 na kubakia watu 3,601,105, sawa na asilimia 37.4 ya watu wote waliokuwepo wakati wa muungano, ikimaanisha wengine wameshakufa au hawapo Tanzania. Kati ya watu hao, wanaume ni 1,642,767 na wanawake ni 1,958,338.
Idadi ya watu waliozaliwa baada ya muungano inakadiriwa kufika 62,046,535 ambapo kati ya watu hao, wanaume ni 30,378,046 na wanawake ni 31,668,489.


Kwa msingi huo, watu wengi waliopo nchini mwaka 2024 wamezaliwa baada ya Muungano. Hii inamaanisha kuwa, ili kuimarisha muungano, hapana budi serikali kuendelea kuongeza jitihada katika kutoa elimu kuhusu historia, umuhimu na kuonesha kwa vitendo mafanikio ya muungano.

Umri wa muungano kwa sasa ni sawa na umri wa mtumishi wa umma anayestaafu kwa lazima kwa mujibu wa sheria. Hivyo basi, wakati Watanzania wakiadhimisha miaka 60 ya kuzaliwa muungano, hawana budi kujivunia mchango mkubwa wa tasnia ya takwimu katika maendeleo ambayo muungano umeifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zenye umoja, amani, utulivu, mshikamano na zaidi uchumi imara unaokua kwa kasi na kuleta matumaini kwa wananchi wake.



Jengo la Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) Zanzibar

# Msuya, Malecela na Mongella *Watoa Neno Muungano Kutimiza Miaka 60*



*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 26 Aprili 1964 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.*

Na Jonas Kamaleki - Dodoma

Tanzania inapoadhimisha miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wawili walipata kuwa mawaziri wakuu na makamu wa kwanza wa rais, Mhe. John Samwel Malecela na Mhe. Cleopa David Msuya, wameeleza kufurahishwa kwao kutokana na kuendelea kuwepo kwa muungano uliodumu kwa muda mrefu.

Akiongea na waandishi wa habari hivi karibuni katika mahojiano maalum yaliyoratibiwa na Idara ya Habari (Maelezo) iliyo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Mhe. John Samuel Malecela, aliuelezea muungano kama ni wa kipekee barani Afrika na duniani, kwa sababu nchi nyingi zilijaribu kuungana lakini zilishindwa na zile zilizoungana hazikudumu.

Mzee Malecela anasema kuwa ni fahari kwa Tanzania kufikisha miaka 60 ya muungano na tumaini la muungano huo kudumu miaka mingi zaidi limebaki kwa vijana ambao ndio nguvu kazi ya sasa. "Sisi Watanzania tumekuwa mfano mzuri; niwaombe vijana ninyi muundeleze muungano huu. Pengine, labda tulikosea hapa na pale lakini muungano bado upo", amesisitiza Mzee Malecela.

Mzee Malecela anaeleza kuwa muungano huu una serikali mbili kwa maana ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini lengo lilikuwa ni kuelekea kuwa na serikali moja; hivyo, angependa kuona muungano unaimarika zaidi na kuwa na serikali moja.



*Kutoka kulia: Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyekuwa Makamu wa Rais Aboud Jumbe, Waziri Mkuu Mstaafu, Cleopa Msuya, Joseph  Nyerere na Aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Sokoine wakiwa Ikulu, jijini Dar es Salaam mwaka 1981.*



*Gertrude Mongella (katikati) ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Kongamano la Nne la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake akiwa katika hafla ya chakula cha mchana kwa waandishi wa habari katika Kongamano hilo Beijing, nchini China tarehe 4 hadi 15 Septemba, 1995.*

"Sisi wazee tulitamani kuona muungano unatoka kwenye serikali mbili tulizo nazo na kuwa serikali moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; hili sisi hatukulifikia lakini ninyi vijana mtalifikia," anasema Mzee Malecela.

Kwa upande wake, Mhe. Cleopa David Msuya, Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, anasema muungano huu umeweza kudumu kutokana na historia ya watu wa pande mbili za muungano kuwa na udugu wa damu; na ndio maana unakuta watu wengi wa Tanzania Zanzibar wana ndugu zao wa damu Tanzania Bara.

"Sababu ya udugu imefanya muungano wetu kuwa imara na kudumu licha ya changamoto chache za muungano zilizokuwa zikijitokeza," anasisitiza Mzee Msuya.

Mzee Msuya anasema ni jambo la kujivunia kama Watanzania tunapoadhimisha miaka 60 ya muungano; kwani si jambo rahisi kufikia hapo ukizingatia nchi nyingi zilijaribu lakini hazikufanikiwa.

Mwanasiasa mkongwe, Balozi Getrude Mongella, anasema muungano huu ni wa udugu zaidi kwani unakuta Pemba kuna watu wana ndugu zao Ukerewe mkoani Mwanza au mkoa wa Katavi na kwamba hali hiyo imeufanya muungano kudumu hadi miaka 60 inayoadhimishwa.

Kwa mujibu wa Balozi Mongella, muungano huu unapaswa kuenziwa na vizazi hadi vizazi na kuwa mfano wa kuigwa si barani Afrika tu bali ulimwenguni kote na kuwamwagia sifa waasisi, Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, aliyekuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar.

Muungano huu ambao uliziunganisha nchi mbili, iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ni wa kipekee na ambao umedumu kwa kipindi kirefu. Baadhi ya nchi zilizowahi kuungana lakini hazikudumu ni Senegal na Gambia mwaka 1982 na kutumia jina la Senegambia kabla ya kuvunjika mwaka 1989; na mataifa ya Misri la Afrika na Syria la Mashariki ya Kati mwaka 1958 na kuvunjika mwaka 1961.

Muungano huu hauna budi kuenziwa na kudumishwa bila kuongeza changamoto. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, ni asilimia 3 tu ya Watanzania ndio waliokuwepo wakati wa muungano unaasisiwa na asilimia 97 ya Watanzania wamezaliwa baada ya muungano.
Kwa mantiki hii hakuna wa kujitokeza kuvunja muungano huu hasa kwa kizazi hiki kilichozaliwa baada yake.
Kama kauli mbiu isemavyo: Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Tumeshikamana na Tumeimarika, kwa Maendeleo ya Taifa Letu, inawafanya Watanzania kuwa imara zaidi na kuuenzi muungano kwa miaka mingi zaidi.

> Sisi Watanzania tumekuwa mfano mzuri; niwaombe vijana ninyi muundeleze muungano huu. Pengine, labda tulikosea hapa na pale lakini muungano bado upo
>
> ***Mhe. John Samwel Malecela***



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimtunuku na kumvalisha Nishani ya Mwenge wa Uhuru Daraja la Pili Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. John Samwel Malecela kwenye hafla iliyofanyika Ikulu ya Chamwino, Dodoma tarehe 24 Aprili, 2024.






*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 26 Aprili 1964 katika Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam.*



# Uchumi wa Jeshi, Maslahi ya Wanajeshi *Yaboreshwa*

Na Mwandishi Wetu

Tunapoadhimisha miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliotiwa saini tarehe 22 Aprili, 1964, na kufuatiwa na matukio mbalimbali ya muungano yaliyohitimishwa rasmi tarehe 26 Aprili, 1964. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), inayo kila sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana katika kipindi husika.

Serikali kupitia wizara hii imefanikiwa kujenga na kuimarisha uchumi wa jeshi; kuboresha maslahi kwa wanajeshi; na watumishi wa umma kadri uwezo wa kifedha unavyoruhusu; kuwapatia makazi bora kwa kuwajengea nyumba askari na kuwapatia maslahi mengine.

Serikali imejenga zaidi ya nyumba 6,000 katika kambi mbalimbali za jeshi kwenye mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Morogoro, Pemba, Pwani na Tanga. Aidha, ujenzi wa nyumba hizo, kwa kiasi kikubwa, umepunguza uhaba wa nyumba pamoja changamoto ya wanajeshi kuishi uraiani.

Vilevile, ujenzi na ukarabati wa baadhi ya miundombinu inayotumiwa na wanajeshi ikiwemo ujenzi wa makao makuu ya ulinzi wa taifa, pamoja na majengo ya huduma kama vile hospitali, mabwalo, mahanga ya kuishi askari makapera na vijana wa JKT, shule, vyuo na ukarabati wa miundombinu mingine pia, umeendelea kufanyika.

Kwa upande wa stahili, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekuwa ikizingatia hali halisi ya mazingira ya kazi katika kutoa stahili mbalimbali kwa wanajeshi wake, kwa wakati na kwa viwango vizuri. Vyeo pia vimeendelea kutolewa kulingana na sifa, vigezo na taratibu zilizopo kisheria. Maboresho mbalimbali ya sheria yamefanyika ikiwemo Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa Na. 16 ya mwaka 1964 (The National Service Act No. 16 of 1964) ambayo iliwezesha kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) hapo tarehe 10 Julai, 1963. Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mbalimbali hadi mabadiliko ya mwaka 2002. Sheria hiyo inampa Mkuu wa JKT, dhamana ya kuandikisha vijana wa kujitolea kwa mujibu wa sheria, kwa ajili ya malezi, uzalishaji mali na ulinzi wa taifa.

Aidha, JKT imeendelea kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali wakiwemo waheshimiwa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata watumishi  wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ili kuwajengea maadili mema, ukakamavu na moyo wa uzalendo. Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, wahitimu hao wamekuwa ni mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ), imeendelea kutoa mafunzo kwa vijana katika mikoa yote ya Tanzania, ambao ni sehemu ya Jeshi la Akiba. Jeshi hili limeendelea kushiriki katika shughuli za ulinzi ndani ya nchi. Vilevile, JWTZ kupitia kamati za usalama za wilaya na mikoa, imeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi na usalama. Aidha, Jeshi la Akiba limepata mafanikio makubwa katika kuwajengea wananchi uzalendo na kuwapatia ujuzi wa kulinda maeneo mbalimbali muhimu, na hivyo kujenga mshikamano wa kitaifa.

Aidha, wizara kupitia taasisi zake imeendelea kufanya na kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa kwa matumizi ya kijeshi na kiraia. Katika kipindi cha miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar, serikali imeanzisha viwanda vya kijeshi ikiwemo kiwanda cha Tanzania Automotive Technology Centre (TATC), maarufu kama Nyumbu, pamoja na Shirika la Mzinga.

Shirika la TATC lilianza mwaka 1977, wakati huo ikijulikana kama Mradi wa Nyumbu. Ilipofika tarehe 14 Desemba, 1985, mradi huu ulibadilishwa jina na kuwa shirika kamili la TATC kwa amri ya Rais chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969; na kuwekwa chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.
Baada ya kuanzishwa kwake shirika hili lilikabidhiwa majukumu makuu saba yakiwemo kufanya utafiti katika teknolojia zilizopo duniani; kufanya usanifu wa magari na mitambo; kutoa ushauri wa kitaalamu kwa viwanda nchini; utafiti wa malighafi kwa ajili ya matumizi katika uhandisi mitambo katika teknolojia ya kuharibu vyuma (foundry engineering).

Kwa upande wa Shirika la Mzinga lilianzishwa mwaka 1971 kama mradi wa mazao ya msingi chini ya makao makuu ya jeshi kwa ajili ya kuzalisha mazao kwa matumizi ya JWTZ. Tarehe 13 Septemba, 1974, mradi huu ulifanywa kuwa Shirika la Umma (Public Corporation) kwa tamko la Serikali Na. 219. Shirika hili limeendelea kutekeleza majukumu ya aina kuu mbili; kwanza, ni shughuli za kuzalisha mazao ya msingi ya mwaka 1971 na mazao yaliyoongezwa mwaka 2012 ambapo uzalishaji wake umeongezeka kutoka asilimia 11 hadi kufikia asilimia 87 mwaka 2022.

Pili, shirika hili pia, linajishughulisha na shughuli za uzalishaji mazao mbadala, ili kujiongezea kipato kwa lengo la kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka serikalini.

Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia JWTZ, imekuwa ni mwanachama wa jumuiya za kikanda, kimataifa, pamoja na ushirikiano wa uwili (bilateral), imeendelea kushirikiana na nchi hizi kupitia nyanja mbalimbali za diplomasia ya kijeshi. Aidha, kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, serikali imeendelea kushirikiana na nchi rafiki kupitia sekta ya ulinzi. Kimsingi ushirikiano huu, unatokana na sera bora ya mambo ya nje ya Tanzania ya mwaka 1964 iliyofanyiwa maboresho mwaka 2020.

Sera hiyo inatamka bayana kuhusu msimamo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kudumisha amani, kuhakikisha usalama wa ndani na nje ya nchi, kudumisha ujirani mwema, pamoja na kusaidia Umoja wa Mataifa katika kufikia lengo lake la kuleta na kudumisha amani kote duniani.

Vilevile Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendeleza kudumisha uhusiano na mataifa mbalimbali duniani; kupitia mafunzo na mazoezi ya kijeshi; misaada ya kitaalam; vifaa, zana na mitambo; ubadilishanaji wa wataalam; ubadilishanaji taarifa za uhalifu unaovuka mipaka; shughuli za ulinzi wa amani; mapambano dhidi ya ugaidi, uharamia baharini, uvuvi haramu; na usafirishaji haramu wa binadamu. Ushirikiano huu, umesaidia kujenga mahusiano mazuri na nchi husika na kuongeza wigo wa mahusiano ya kijeshi na kutekeleza kwa vitendo makubaliano mbalimbali ya ulinzi wa amani.



# Kamati ya Pamoja SMT, *SMZ Nguzo Muhimu kwa Uhai wa Muungano*

Na Mwandishi Wetu

Muungano unaweza kuelezwa kuwa ni kitendo cha nchi mbili au zaidi kuachia na kukabidhi mamlaka yao yote au baadhi kwa serikali moja kuu itakayotekeleza mamlaka hayo kwa masharti mahsusi ya kikatiba.

Lengo kuu la muungano ni kuunganisha nguvu katika maeneo yote au maeneo mahsusi ili kuchochea tija kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiulinzi, kiusalama na pia katika ushirikiano na nchi mbalimbali duniani.

Pamoja na faida mbalimbali zinazotokana na muungano, changamoto mbalimbali hujitokeza ambapo kama hazitafanyiwa kazi kikamilifu zinaweza kutishia uhai wa muungano wowote ule, iwe ni muungano jumuishi, muungano wa shirikisho au muungano shirikisho maalum.

Kwa mujibu wa kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo, uhai wa muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na utaratibu uliowekwa wa serikali za pande zote mbili za muungano wa kutatua changamoto za muungano kupitia mfumo rasmi wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya muungano.

Mfumo huu wa vikao umeboresha utaratibu na kuongeza kasi ya utatuzi wa hoja za muungano. Kamati hii iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imeweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao unaoshirikisha viongozi na wataalamu kutoka SMT na SMZ, ambavyo hufanyika katika ngazi tatu za Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ, Mawaziri wa SMT na SMZ na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tangu kamati hii ianze kazi mwaka 2006, hoja 25 za muungano ziliibuliwa ambapo hadi kufikia Februari 2024, hoja 22 zilijadiliwa, kupatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za kero za muungano. Kwa hiyo zimebakia hoja tatu tu.

Aidha, kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo, kinaeleza kuwa pamoja na kuwepo kwa kamati ya SMT na SMZ, kumekuwa na ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye masuala yasiyo ya muungano, ambapo serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa wizara, idara na taasisi zisizo za muungano kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kwa manufaa ya Watanzania.

Waswahili wanasema "ukiona vinaelea basi ujue vimeundwa", ndivyo ilivyo kwa muungano wetu ambapo Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ imekuwa ikifanyia kazi hoja mbalimbali za muungano na kuufanya muungano huu kuwa ni wa kipekee na wa mfano duniani, ambapo tarehe 26 Aprili, 2024, unatimiza miaka 60 huku ukiongozwa na kauli mbiu isemayo: Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano: Tumeshikama na Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa Letu.





# Ijue Misingi ya *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar*

Na Mwandishi Wetu

Historia inaonesha kuwa siyo jambo rahisi kuunganisha nchi mbili au zaidi kwa nia njema ya kupata nguvu ya pamoja ili kuimarisha ulinzi na usalama na kuchochea tija kwenye nyanja zote za maendeleo.

Kumekuwa na jitihada za nchi mbalimbali za kuungana barani Afrika lakini jitihada hizo hazikuweza kudumu na kuzaa matunda ya muungano. Mfano wa nchi zilizowahi kuungana au kufanya jaribio la kuungana lakini zikashindwa au muungano kuvunjika, ni Shirikisho la Ethiopia na Eritrea mwaka 1952. Shirikisho hilo lilivunjika mwaka 1993 kufuatia ukiukwaji wa masharti ya shirikisho na baada ya kura ya maoni kuamua hivyo.

Shirikisho la Mali ambalo lilihusisha nchi za Senegal na Mali kipindi cha ukoloni wa Ufaransa. Shirikisho hilo lilivunjika miezi miwili tu baada ya nchi hizo kupata uhuru, huku mivutano ya kisiasa kuhusu itikadi, misingi ya shirikisho pamoja na changamoto iliyojitokeza ya Ufaransa kuendelea kuwa na kituo cha kijeshi nchini Mali, zikielezwa kuchangia kuua muungano wa Senegal na Mali.

Muungano wa Shirikisho la Rhodesia (Zimbabwe na Zambia) na Nyasaland (Malawi) nao lilivunjika miezi michache tu kabla ya uhuru wa Malawi na Zambia mwaka 1964. Shirikisho la Senegambia lilianza Februari 1, 1982, na kuhusisha nchi za Senegal na Gambia, lakini lilidumu kwa miaka saba tu na kuvunjika mwaka 1989.

Muungano maalum wa Ghana, Guinea na Mali ulionzishwa mwaka 1958 nao uligonga mwamba na kusambaratika mwaka 1963 kutokana na mivutano ya dhana nzima ya muungano barani Afrika.

> “Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar umeendelea kudumu na unatarajiwa kudumu kwa miaka mingine zaidi, kutokana na misingi imara iliyowekwa, ambayo imekuwa ikitoa ufumbuzi wa kudumu wa changamoto na hoja za muungano pale zinapojitokeza.

Mfano wa muungano mwingine ambao nao haukudumu kama ilivyo kwa nchi zingine, ni muungano wa Misri na Syria. Muungano huu ulianzishwa mwaka 1958 na ulidumu kwa miaka 13 tu kabla ya kuvunjika mwaka 1961, kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo Serikali ya Misri kupinduliwa kijeshi na pia manung’uniko ya mshirika mmoja kutoridhika na mgawanyo wa madaraka

Mifano hiyo inaonesha namna ambavyo si kazi rahisi kwa muungano kudumu muda mrefu tofauti na muungano wetu ambao umedumu na utatimiza miaka 60 ifikapo Aprili 26, 2024, na kwa mujibu wa kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo, misingi mikuu ya muungano kudumu ni kama pamoja na:

### *Mazingira rafiki na wezeshi*

Kuwepo kwa mazingira rafiki na wezeshi kwa maana ya ujirani na ukaribu wa wanamuungano kijiografia; utambulisho unaofanana au kushabihiana; kuwa na mapito ya kihistoria ya pamoja; na kuwa na utashi na matarajio yanayofanana ya wananchi.

Kihistoria, watu wa Tanzania Bara na Zanzibar wana historia ya pamoja ya karne nyingi za ustawi bila kuingiliwa na wageni na historia ya pamoja ya miongo mingi ya ukoloni, utumwa na mapambano ya ukombozi.

Kijiografia inaonesha Tanzania Bara na Zanzibar ni karibu, na ujirani huu ndio ulioruhusu mwingiliano rahisi na mkubwa kati ya watu wa bara na visiwani kwa karne nyingi katika kutafuta fursa za kibiashara na maeneo mapya na mazuri ya kuishi.



*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 26 Aprili 1964 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.*



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume (kulia) wakibadilishana Hati za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 27 Aprili, 1964.*

Lugha ya Kiswahili nayo ilikuwa kiunganishi muhimu ambayo ilishika kasi na kuwa lugha kuu ya kiserikali, kibiashara na katika mawasiliano ya mtu na mtu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kiswahili kimewaunganisha wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa jamii moja.

### *Msimamo, kauli na matendo ya viongozi*

Misimamo, kauli na matendo ya viongozi kushabihiana na utashi na matarajio ya wananchi juu ya muungano na kuyaishi kisheria na kikatiba. Viongozi wa kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapokabidhiwa madaraka kuiongoza nchi wanakula kiapo cha kuihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutetea na kudumisha umoja kwa mujibu wa hiyo. Kwa Watanzania muungano ni sehemu ya tunu ya taifa ya umoja ambayo viongozi hawana budi kuiishi au kufanana nayo katika kauli na matendo.

### *Uwiano katika mgawanyo wa madaraka na ustawi*

Haya ni moja ya masuala makubwa ya muungano ambayo Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliyahubiri kwa muda mrefu na kuacha nasaha nzito miongoni mwa wananchi, ni hadhi ya Zanzibar kama nchi iliyoungana na Tanganyika kuunda Tanzania na uhuru wake kwenye mambo yasiyokuwa ya muungano.


Kwa mujibu wa Baba wa Taifa, suala lolote la muungano lazima liwe na ushiriki wa pande zote mbili kwa uzito unaolingana hata kama idadi ya washiriki itatofautiana kwa idadi ya uwakilishi.

### *Ustarabu mahususi wa kupokea changamoto au hoja na njia rasmi za utatuzi wake*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu wa serikali za pande zote mbili za muungano kutatua changamoto na hoja za muungano kupitia mfumo rasmi wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya muungano.

Kamati hii iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imeweka utaratibu wa uendeshaji wa vikao unaoshirikisha viongozi na wataalamu kutoka SMT na SMZ, ambavyo hufanyika katika ngazi tatu za Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ, Mawaziri wa SMT na SMZ na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa lengo la kuhakikisha hoja zote za muungano zinazoibuliwa zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.


Muungano wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar umeendelea kudumu na unatarajiwa kudumu kwa miaka mingine zaidi, kutokana na misingi imara iliyowekwa, ambayo imekuwa ikitoa ufumbuzi wa kudumu wa changamoto na hoja za muungano pale zinapojitokeza.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar ikiwa ni ishara ya kuunganisha nchi mbili wakati wa Sherehe ya Muungano Dar es Salaam tarehe 26 Aprili, 1965.



Matukio mbalimbali katika picha wakati wa sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tarehe 26 Aprili 1964 katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.



# *Miaka 60 ya Muungano* Yazipa Nguvu Sekta za Viwanda na Biashara

Na Suzan Mshakangoto, WVB

Tanzania sasa imefikisha miaka 60 ya muungano huku sekta za viwanda na biashara zikiwa miongoni mwa wanufaika na muungano huo kwa kutengeneza soko kubwa la pamoja lenye watu takriban milioni 65, ambalo limeongeza fursa za biashara, ajira na kukuza uchumi wa taifa na wananchi wake.

Fursa zinazotokana na muungano huu ni pamoja na kuongezeka kwa biashara kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo wafanyabiashara wa Tanzania Bara wamesafirisha bidhaa zao moja kwa moja Zanzibar bila vikwazo vya kibiashara na vivyo hivyo kwa wazalishaji wa Zanzibar kuuza bidhaa zao Tanzania Bara na hatimaye kukuza biashara na uchumi wa pande zote mbili za muungano.

Aidha, muungano umeiwezesha Tanzania kuanzisha viwanda vingi vinavyotengeneza bidhaa mbalimbali zinazotosheleza mahitaji ya ndani na nje ya nchi. Hii imechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuinua maisha ya wananchi. Hivyo, muungano huu umeunganisha nguvu na rasilimali za pande zote mbili na kuzalisha fursa mpya ambazo hazikuwepo awali.
Muungano pia umeiwezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano wake katika majadiliano ya biashara ya kikanda na kimataifa ambapo nchi imeridhia kuingia mikataba mbalimbali ya kibiashara kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), Shirika la Biashara la Dunia (WTO), Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Biashara na Maendeleo (UNCTAD) na mingineyo. Kupitia mikataba hii, Tanzania imefanikiwa kutetea maslahi yake na kupata fursa mpya za biashara na uwekezaji kwa kuzingatia maslahi ya pande zote mbili za muungano.

Katika kuonesha kuwa muungano wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar una umuhimu mkubwa, walisisitiza umuhimu wake katika kuendeleza sekta mbalimbali zikiwemo za viwanda na biashara.


Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mwaka 1967 alisema: "Muungano wetu ni mfano bora wa ushirikiano wa Afrika. Tumeonyesha kwa vitendo kuwa umoja ndio nguvu." Mwaka 1995 akasema: "Muungano wetu umetuwezesha kujenga uchumi imara zaidi. Kwa pamoja, tumefanikiwa kuanzisha viwanda vingi vinavyotengeneza bidhaa mbalimbali zinazotosheleza mahitaji ya ndani na nje ya nchi."

Naye Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi, Hayati Abeid Aman Karume, mwaka 1964 alisema: "Muungano umetufungulia milango ya fursa mpya za kiuchumi. Kwa pamoja, tunaweza kujenga uchumi imara na unaostawi."  Na mwaka 1967 alinukuliwa akisema kuwa muungano ni nguzo muhimu ya umoja wa Afrika na kwamba kuungana kwa mataifa mawili, kunaonesha mfano bora wa ushirikiano na maendeleo kwa bara zima la Afrika."

Kwa miaka 60 sasa, muungano huu umeleta ustawi mkubwa nchini Tanzania, hasa katika sekta ya viwanda na biashara. Mfano, kabla ya muungano, Zanzibar ilijulikana kama kisiwa cha viungo, ikisafirisha viungo kama karafuu, pilipili nyeusi na vingine duniani kote. Tanganyika kwa upande wake, ilikuwa na ardhi yenye rutuba, ikizalisha mazao kama pamba, kahawa, chai na tumbaku.

Muungano umefungua fursa mpya za ushirikiano katika maendeleo ya viwanda. Kwa mfano, Zanzibar inasambaza karafuu kwa viwanda vya sabuni na vipodozi vya Tanzania Bara, wakati Tanzania Bara nayo inasambaza nguo, bidhaa za chuma na vifaa vya ujenzi huko Zanzibar. Hii imeimarisha uchumi wa pande zote mbili na kupunguza utegemezi wa uagizaji kutoka nje ya nchi.

Aidha, Tanzania imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani na kwa mujibu wa takwimu kutoka katika kitabu cha hali ya uchumi cha mwaka 2022, uzalishaji wa bidhaa za sigara, nyavu za uvuvi, bia, saruji, dawa za pareto, bati, chuma na rangi uliongezeka kutokana na mahitaji ya bidhaa hizo katika soko.



Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli akisalimiana na NaibuWaziri wa Biashara kutoka Jamhuri ya Watu wa China, Ndg. Qian Keming Ikulu, jijini Dar es Salaam tarehe 14 Oktoba, 2016.



Rais wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akizungumza katika Jukwaa la Uchumi Duniani (World Economic Forum -WEF), Davos nchini Uswizi tarehe 26 Januari 2012. *(Picha na  Matthew Jordaan, Mediapix)*

Aidha, Tanzania imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani na kwa mujibu wa takwimu kutoka katika kitabu cha hali ya uchumi cha mwaka 2022, uzalishaji wa bidhaa za sigara, nyavu za uvuvi, bia, saruji, dawa za pareto, bati, chuma na rangi uliongezeka kutokana na mahitaji ya bidhaa hizo katika soko.

Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Ali Hassan Mwinyi, alisisitiza umuhimu wa muungano katika kuendeleza sekta ya viwanda na biashara ambapo mwaka 1985 alinukuliwa akielezea umuhimu wa muungano: "Muungano umeimarisha ushirikiano wetu katika sekta ya viwanda. Tunashirikiana kuzalisha bidhaa ambazo zinatufaidisha sote," alieleza Hayati Mwinyi; na kuongeza kwamba muungano umewezesha kupatikana kwa masoko mapya ya bidhaa ndani na nje ya nchi na hivyo kusaidia kukuza uchumi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais wa tatu wa Tanzania, Mhe. Hayati Benjamin Mkapa, naye alizungumzia umuhimu wa muungano. Mwaka 1995, alisema: "Muungano ni tunu ya thamani ambayo tunapaswa kuilinda na kuithamini. Kwa pamoja, tumeweza kufikia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali, ikiwemo sekta ya viwanda na biashara." Aidha, mwaka 2000, Hayati Mkapa aliongeza kwa kusema: "Muungano umetuwezesha kuingia katika soko la dunia kwa ufanisi zaidi. Sasa tunasafirisha bidhaa zetu kwa nchi mbalimbali duniani kote."

Kwa mujibu wa kitabu cha hali ya uchumi cha 2022, takwimu zinaonyesha thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka Tanzania iliongezeka katika kipindi cha miaka 60 ya muungano hadi kufikia dola za Marekani milioni 7,223.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa asilia hususan korosho na tumbaku pamoja na bidhaa zisizo asilia ikiwemo bidhaa za viwandani, dhahabu na makaa ya mawe.

Aidha, mauzo ya bidhaa zisizo asilia yalichangia asilimia 83.9 ya mauzo yote nje ya nchi; bidhaa asilia zilichangia asilimia 10.6 na bidhaa zisizorekodiwa asilimia 5.5. Mafanikio haya yote yanatokana na muungano imara ulioasisiwa mwaka 1964, unaojenga misingi imara ya ufanyaji biashara na uzalishaji viwandani.

Aidha, katika kipindi cha miaka 60 ya muungano, kufikia mwaka 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa asilia nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 766.5. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, tumbaku, pamba na katani kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya nje na uzalishaji wa ndani.

Kwa miongo sita iliyopita, muungano huu umeonesha jinsi umoja na ushirikiano unavyoweza kuleta maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara. Ushirikiano kati ya pande zote mbili umeimarisha uchumi wa Tanzania na kuboresha maisha ya wananchi wake.

Rais wa nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, naye alinukuliwa mwaka 2005 akisema: "Muungano ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Tanzania. Kwa pamoja, tumeweza kujenga uchumi imara na unaokua kwa kasi." Pia mwaka 2010 alinukuliwa akisema: "Muungano umetufungulia fursa mpya za ushirikiano na nchi nyingine za Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika."
Kwa upande wake, Rais wa Awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, katika kuonyesha umuhimu wa muungano katika sekta ya viwanda ambapo mwaka 2015 alisema: "Muungano ni mfano bora wa umoja wa Afrika. Tumeonyesha kwa vitendo kuwa tunaweza kushirikiana na kufanikiwa pamoja."

Kwa upande wake, Rais wa Awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, katika kuonyesha umuhimu wa muungano katika sekta ya viwanda ambapo mwaka 2015 alisema: "Muungano ni mfano bora wa umoja wa Afrika. Tumeonyesha kwa vitendo kuwa tunaweza kushirikiana na kufanikiwa pamoja."
Naye Rais wa Awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliuelezea muungano kama ni tunu yenye thamani na hivyo ni lazima kuendelea kushirikiana na kusaidiana ili Tanzania iweze kufikia malengo ya maendeleo. "Muungano ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Tunafanya kazi pamoja ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinasambazwa kwa usawa na kila mtu anafaidika," alisisitiza Rais Samia.
Mwaka 2020, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, alinukuliwa akisema: "Tunahimiza sekta binafsi ya Tanzania Bara na Zanzibar kushirikiana katika kuanzisha viwanda vipya na kuimarisha biashara kati ya pande zote mbili."

Nukuu za viongozi wote hao zinaonyesha wazi umuhimu wa muungano wa katika maendeleo ya sekta ya viwanda na biashara. Marais wote wa Tanzania wamesisitiza faida za muungano na wametoa wito wa kuendeleza ushirikiano kati ya pande zote mbili. Aidha, muungano umeleta mafanikio makubwa katika nyanja ya mtangamano wa biashara ambapo pande zote mbili za muungano pia zimefanikiwa katika kuendeleza ushirikiano katika matumizi ya fursa za mafunzo zinazotolewa na Shirika la Biashara la Dunia (WTO) ambapo maafisa kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamekuwa wakishiriki kikamilifu katika mafunzo hayo ambayo yamekuwa yakisaidia katika kuongeza ujuzi na maarifa na kuboresha utendaji kazi.

Pamoja na msisitizo uliotolewa na viongozi hao, sasa sekta binafsi hususani wajasiriamali wadogo wananufaika katika kukuza na kuendeleza biashara zao, kwa kushirikiana katika upatikanaji wa malighafi katika pande zote mbili na upatikanaji wa soko la bidhaa hizo pamoja na miradi mbalimbali inayoendeshwa na serikali katika kuwasaidia wajasiriamali hao.

Katika kuthibitisha hilo, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia WTO, ilitekeleza mradi ujulikanao uliolenga kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati kuanzia mwaka 2020–2022 kwa pande zote, Tanzania Bara na Zanzibar.

Mradi huo ulifanikiwa kuwawezesha wajasiriamali walio kwenye mnyororo wa thamani wa zao la dagaa (mkoa wa Kaskazini Unguja), mwani (Mkoa wa Kaskazini Pemba), chikichi (Kigoma Vijijini na Uvinza), asali (Itigi, Singida) na mbogamboga na matunda wilayani Bunda mkoani Mara, na wilaya ya Busega mkoani Simiyu, ili waweze kuzalisha bidhaa zao kwa viwango vyenye ubora wa kimataifa pamoja na kupata masoko ya uhakika kwa bidhaa mbalimbali zinazotokana na mazao hayo na hatimaye kuyafikia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

Wakizungumzia namna Tanzania Bara na Zanzibar zinavyoshirikiana, Mhe. Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji, anasema "Tunahimiza ushirikiano kati ya wafanyabiashara wa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa ufanisi zaidi na kuingia katika soko la kimataifa kwa pamoja."



Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa akihutubia mjadala mkuu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 21 Septemba 2004 jijini New York, Marekani. *(Picha na Getty Images)*

Kwa upande wake, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shaban Omary, anasema: "Tunaendelea kushirikiana kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji pande zote mbili za muungano ili kuvutia wawekezaji zaidi na kukuza uchumi wetu".

Haya yanathibitishwa na mafanikio ya muungano ambao umefungua milango ya ushirikiano katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya viwanda na biashara pamoja na taasisi zake kama vile Wakala wa Vipimo (WMA) na Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS) ambazo zinaendelea kuboresha viwango vya bidhaa nchini Tanzania.

Ushirikiano katika nyanja ya viwanda umewezesha Tanzania kujenga viwanda vipya vinavyotumia rasilimali za pamoja, kuboresha ubora wa bidhaa na kupunguza utegemezi wa uagizaji kutoka nje. Soko la pamoja limewezesha bidhaa za Tanzania kuuzwa kwa urahisi katika nchi zote mbili na kuongeza mauzo na mapato kwa wafanyabiashara.

Hivyo tunaweza kusema miaka 60 ya Muungano, imeleta mafanikio makubwa katika sekta ya viwanda na biashara, kutengeneza soko la pamoja lenye watu zaidi ya milioni 60 na hivyo kufungua milango ya fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa pande zote mbili. Muungano huu utaendelea kuwa nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi kwa miaka mingi ijayo.



Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ali Hassan Mwinyi akikagua gwaride Addis Ababa, nchini Ethiopia alipowasili nchini humo kuhudhuria mkutano wa 23 wa Umoja wa Muungano wa Afrika (OAU) tarehe 24 Julai, 1987. *(Picha na Alexander Joe, Getty Images)*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan*



# Miaka 60 ya Muungano
## *Imewanufaisha Watanzania Kijamii, Kimazingira, Kisiasa na Kiuchumi*

Na Mwandishi Wetu

Tarehe 26 Aprili, 2024, nchi yetu inaadhimisha miaka 60 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar tangu kuasisiwa kwake.
Waasisi wa taifa letu, Hayati Sheikh Abeid Amani Karume na Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, walifanya kitendo cha kishujaa na kihistoria cha kuziunganisha nchi zetu mbili na kuwa nchi moja ijulikanayo kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunapoadhimisha miaka 60 ya muungano huu, Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia muungano wetu kutokana na matunda na mafanikio lukuki yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 60.
Waasisi hao waliweka misingi ya umoja, amani, mshikamano na utulivu kutokana na sehemu kubwa ya mizizi ya muungano huo kujikita kwa wananchi pamoja na umakini na usikivu wa viongozi wakuu wa serikali zote mbili, yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Kutokana na uimara wa misingi hiyo, sote tumeshuhudia mafanikio lukuki katika kipindi cha miaka 60 ya muungano kwenye nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mafanikio haya yanajumuisha uhuru wa wananchi kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo popote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimefanikiwa kusimamia utekelezaji wa masuala ya muungano kwa ufanisi mkubwa kutokana na sera imara pamoja na uwekezaji katika miundombinu wezeshi kwa ajili ya ukuaji wa kiuchumi ikiwemo nishati, usafiri na usafirishaji.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia zimeendelea kushirikiana katika kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imechangia kupunguza umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii kwa wananchi wake.

Miongoni mwa miradi na programu zilizotekelezwa katika pande zote mbili za muungano na kukamilika ni: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa awamu ya kwanza, pili na tatu (TASAF I, TASAF II na TASAF III); Programu ya Usimamizi wa Bahari na Pwani (MACEMP); Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP); na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo na Sekta ya Mifugo (ASDP-L).

Miradi na programu zingine ni Programu ya Kuwezesha Sekta ya Kilimo (ASSP); Programu ya Changamoto za Milenia (MCA-T); Mradi Shirikishi wa Programu za Maendeleo ya Kilimo (PADEP); Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH); Programu ya Miundombinu ya Masoko; Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini (MIVARF); na Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (ERPP).



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia akiwa amekaa kwenye Chumba cha Marubani ya Ndege mpya ya Mizigo aina ya Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania ATCL mara baada ya kuizindua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam tarehe 03 Juni, 2023.

Aidha, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na: Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia ya Vijijini (EBARR); Mradi wa Daraja la Kuvukia na Matuta Mawili ya Kuzuia Maji ya Bahari na Mvua (Sipwese) Pemba; na Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania (LDFS).

Pia serikali hutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kupitia mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo kwa majimbo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Majimbo ya Zanzibar hupokea takribani shilingi bilioni 1.4 kila mwaka ambazo hutumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika majimbo 50 yaliyopo Zanzibar.

Katika kuhakikisha muungano wetu unaendelea kuwa imara na madhubuti, serikali za pande zote mbili za muungano zimeweka utaratibu wa wazi na huru wa vikao vya pamoja kwa ajili ya kujadili hoja za muungano na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kuunda tume na kamati mbalimbali kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa hoja zinazoibuliwa kwa lengo la kushauri hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa.

Aidha, kupitia vikao vya kamati ya pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya muungano, serikali zote mbili zimekuwa zikifanya vikao vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za muungano. Tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu mwaka 2006, hoja 25 zimepokelewa na kujadiliwa; na kati ya hizo hoja 22 zimepatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za za kero za muungano.

Pia umeandaliwa mwongozo wa vikao vya kuimarisha ushirikiano kati ya wizara, idara na taasisi zisizo za muungano za serikali zote mbili zinazoshabihiana kimajukumu na zinatakiwa kufanya vikao vya ushirikiano visivyopungua viwili kwa mwaka. Mpaka sasa sasa jumla ya vikao 245 vya ushirikiano vya sekta mbalimbali vimefanyika katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2024.

Elimu kwa umma kuhusu masuala ya muungano imeendelea kutolewa kupitia vipindi vya redio na runinga, makala za magazetini, semina, warsha, makongamano, maonesho ya kitaifa, ziara za viongozi, machapisho mbalimbali na mitandao ya kijamii.
Aidha, elimu kwa umma imekuwa ikitolewa pia kupitia kitabu cha historia ya muungano kijulikanacho kwa jina la ***"Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo"***, ambapo nakala ngumu zilisambazwa kwa wananchi na taasisi za serikali na nakala tete kuwekwa kwenye tovuti ili kurahisisha upatikanaji wa kitabu hicho. Aidha, kitabu hicho kimepata ithibati kwa ajili ya kutumika kama kitabu cha ziada katika shule za sekondari nchini.

## *Mafanikio katika Mazingira*

Tangu kuasisiwa kwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza na kuratibu shughuli ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha panakuwepo na matumizi sahihi ya rasilimali asili na maendeleo endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Idara ya Mazingira ilianzishwa mwaka 1992 ikiwa ni juhudi za serikali kuhimiza uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini, kama ilivyohimizwa na Azimio la Rio mwaka 1992 linalozitaka nchi zote duniani kutambua uhusiano uliopo kati ya maendeleo na mazingira.

Kufuatia kuanzishwa kwa Idara ya Mazingira, Tanzania iliridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira, ambapo katika kutekeleza Azimio la Rio la mwaka 1992, Tanzania iliandaa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Action Plan – NEAP) mwaka 1994.

Kuanzia wakati huo, Sera ya Mazingira ya mwaka 1997, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191, programu, mikakati, mipango na miongozo mbalimbali ya kitaifa ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira imekuwa ikiandaliwa na kutekelezwa. Katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, jumla ya sheria ndogo 326 zimeandaliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Pwani na Ruvuma.

Aidha, kuanzia mwaka 2012 hadi sasa takribani vyeti 2,812 vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na vyeti 1,534 vya ukaguzi wa mazingira vilitolewa kwa miradi mbalimbali. Vilevile, vyeti vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati 17 vilitolewa kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza sera, mipango na miradi ya kimkakati.

Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ambapo mafanikio makubwa yamepatikana katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti nchini ambapo katika kila halmashauri ya wilaya imeelekezwa kwa kupanda ya miti milioni 1.5 kila mwaka.

Aidha, ofisi imeendelea kutekeleza mipango na miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwemo mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi ambao ulitekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar ukifadhiliwa na Mfuko wa Nchi Zinazoendelea (LDCF) kwa thamani ya dola za Marekani milioni 3.3. Lengo la mradi huu ni kuwezesha jamii za watu wa mikoa ya pwani ya nchi kuhimili mabadiliko ya tabianchi hasa yale yanayotokana na kuongezeka kwa kina cha bahari.

Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2012 na kukamilika mwaka 2019 ambapo shughuli zilizotekelezwa na mradi huu ni pamoja na kuendesha mafunzo ya mabadiliko ya tabianchi kwa wataalam zaidi ya 80 wa halmashauri za wilaya za Rufiji, Pangani, Bagamoyo pamoja na wilaya za Zanzibar.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na upandaji wa hekta 1,250 za miti ya mikoko (Rufiji 1,000, Zanzibar 240 na Pangani 10); ujenzi wa ukuta wa kisiwa Panza-Pemba wa mita 40; ujenzi wa ukuta wa Pangani wa mita 950; ujenzi wa makinga bahari matano (5) yenye urefu wa mita 100 kila moja katika eneo la Kilimani-Unguja ili kuzuia mmomonyoko wa fukwe za bahari katika maeneo hayo.

Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa katika upande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza uhakika na usalama wa chakula katika maeneo kame ya Tanzania ambao unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD).


Mradi huu unatekelezwa katika halmashauri tano za Magu (Mwanza), Nzega (Tabora), Mkalama (Singida), Kondoa (Dodoma) na Micheweni (Kaskazini Pemba), ambapo unategemea kuongoa hekta 9,000 za ardhi zilizoharibika katika vijiji 15 vilivyoko katika maeneo hayo ya halmashauri kwa upande wa Tanzania Bara na shehia nane katika halmashauri ya Micheweni.

Lengo la Mradi huu ni kuboresha usimamizi endelevu na kuwezesha urejeshwaji wa mifumo ya ikolojia iliyoharibika ambayo inachangia kutoa huduma muhimu za uzalishaji kwenye maeneo ya ardhi, maji, misitu na bionuai kwa madhumuni ya kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula.

Mradi mwingine ni mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini (EBBAR) ambao unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) wenye thamani ya dola za Marekani milioni 7.57 na kutekelezwa katika wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A (Unguja). Lengo la mradi ni kuongeza uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini, kwa kuimarisha mifumo ya ikolojia na shughuli mbadala za kujiongezea kipato.

Tangu kuasisiwa kwa muungano wetu miaka 60 iliyopita, kumekuwa na faida nyingi zinazoufanya muungano wetu uendelee kuimarika na kushamiri na msukumo na kipaumbele cha uhifadhi na usimamizi wa mazingira ukiendelea kutolewa na viongozi wakuu wa serikali, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi.






Kitabu cha Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akimpa Rais Mstaafu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein vitabu vya Miaka 60 ya Historia ya Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Kitabu cha Safari za Picha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka 60 kwenye hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma tarehe 24 Aprili, 2024.












*Matukio mbalimbali katika picha wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika katika Uwanja wa Uhuru leo Aprili 26, 2024 jijini Dar es salaam.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasili na kukagua gwaride maalumu la maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hafla iliyofanyika Uwanja wa Uhuru leo Aprili 26, 2024 jijini Dar es salaam*

# Tuna Kila Sababu ya Kujivunia Muungano - Rais Samia

Na Lilian Lundo na Jonas Kamaleki, Maelezo

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema Watanzania wana kila sababu ya kujivunia muungano, kwani umetokana na maamuzi ya Watanzania wenyewe.

Samia amesema hayo wakati akihutubia kwenye kilele cha maadhimisho sherehe za miaka 60 ya muungano zilizofanyika Aprili 26, 2024 kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

“Tuna kila sababu ya kujivunia muungano wetu. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetokana na maamuzi yetu wenyewe, tuna makabila zaidi ya 120, imani za dini tofauti tofauti lakini tunaunganishwa na lugha moja ya Kiswahili. Tumeitunza na kuilinda nchi yetu kwa kudumisha amani na utulivu. Tuna kila sababu ya kujivunia muungano wetu,” ameeleza Rais Samia.

Ameendelea kusema kuwa, katika kuendeleza muungano, Watanzania hawana budi kuitekeleza falsafa ya maridhiano, kustahimiliana, kuleta mageuzi na kujenga nchi yetu (4R), kwani italeta maendeleo endelevu katika nchi ili kufikia uchumi wa kati ngazi ya juu.

Aidha, Mhe. Rais ametoa wito kwa Watanzania kuendelea kufanya kazi kwa bidii na maarifa zaidi ili kukuza tija kwa ustawi wa taifa, kwani kazi ndiyo kipimo cha utu.

Baraza la Mapinduzi, amesema kuwa hatua iliyofanywa waasisi wa muungano, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume, ya kuziunganisha iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na kuwa taifa moja la Tanzania, ilikuwa na dhamira ya kuimarisha udugu wa damu na wa kihistoria wa wananchi wa nchi hizi mbili. "Tukiwa tunaadhimisha miaka 60 ya muungano, tuna wajibu wa kumshukuru Mungu kwa mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imeyapata katika sekta mbalimbali na kuendelea kupata sifa na heshima kimataifa kutokana na muungano huu, na kuwa nchi ya kupigiwa mfano kwa muungano huu kudumu, huku kukiwa na amani, umoja na mshikamano", ameeleza Rais Mwinyi.

Amewashukuru viongozi wa awamu zilizopita kwa jitihada zao za kudumisha na kuendeleza malengo ya muungano wa Tanzania na kuzifanyia kazi changamoto za muungano, ni jambo la faraja na kutia moyo kuona changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi.

"Kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar, ninawaahidi Watanzania wenzetu kuwa tutaendelea kuwa waumini wa dhati wa muungano wetu na tutahakikisha unadumu, unaendelea na unazidi kuimarika kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye", alisema Dkt.  Mwinyi.

Naye Rais wa Burundi, Mhe. Evariste Ndayishimiye, ameuelezea muungano wa ndio sababu ya nchi yake kushiriki kilele cha maadhimisho hayo. "Kabla ya wakoloni kufika kwetu, waha, waangaza na Warundi walikuwa ndugu, Warundi na Watanzania walikuwa wakitembeleana. Mpaka wa Burundi na Tanzania umeletwa na mkoloni lakini mpaka sasa Watanzania wa Kigoma na Kagera huwezi kuwatofautisha na Warundi", amesema Rais Ndayishimiye.

Amesema mpaka baina ya Burundi na Tanzania uliowekwa na wakoloni ulikuwa ni kwa ajili manufaa yao, lakini kwa upande wetu umoja umebakikuwa imara na kwamba furaha ya Watanzania ni furaha ya Warundi na kuipongeza Tanzania kwa kufikisha miaka 60 ya muungano.

Sherehe miaka 60 ya muungano zimehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania. Viongozi hao ni Mhe. Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi; Mhe. Azali Assoumani, Rais wa Umoja wa Comoro; Mhe. Hakainde Hichilema, Rais wa Jamhuri ya Zambia na Mhe. Felix Tshisekedi, Rais wa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo.

Viongozi wengine ni Mhe. Hassan Sheikh Mohamud, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Somalia; Mhe. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya; Mhe. Nangolo Mbumba, Rais wa Jamhuri ya Namibia; Mhe. Saulos Chilima, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Malawi; Mhe. Jessica Alupo, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Uganda; Mhe. Adriano Maleiane, Waziri Mkuu wa Msumbiji na Mhe. James Kabarebe, Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwasili na kukagua gwaride maalumu la maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hafla iliyofanyika Uwanja wa Uhuru leo Aprili 26, 2024 jijini Dar es salaam*






MIAKA 60 YA
WA TANZANIA
1964-2024

**Nchi Yetu**




*Tufuatilie katika kurasa zetu kwenye mitandao ya jamii*

/ Msemaji Mkuu wa Serikali
/Maelezo News

Idara ya Habari MAELEZO
S.L.P. 25 Dodoma, Tanzania
Simu: +255 22 292192
Barua pepe:maelezo@mawasiliano.go.tz
www.maelezo.go.tz